# FAMILIA ZA KIAFRIKA KATIKA NJIA PANDA: MITAGUSANO NA CHANGAMANO *ZA* USASA KATIKA *MHANGA NAFSI YANGU* S.A MOHAMMED

**NA**

**JACKLINE KAVIVI MUNYOKI**

**IDARA YA ISIMU NA LUGHA**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**NOVEMBA, 2015**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

______________________________ ________________________

**Munyoki Jackline Kavivi** **Tarehe**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu cha Nairobi.

______________________________ __________________________

**Dkt. Omboga Zaja** **Tarehe**

______________________________ __________________________

**Dkt. Amiri Swaleh** **Tarehe**

# KUTABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia aila yangu. Kwanza ni wazazi wangu wapendwa Bw. na Bi. Patrick Mwiwa kwa kuniombea na kunipa nguvu niendelee na ari yangu ya kusoma hadi upeo wa juu kabisa Mola akinijalia. Pili,kwa ndugu zangu kwa kunipa moyo na matumaini katika kazi yangu, sitawatoa kwenye kumbukumbu zangu kwa mchango wao mkubwa walionipa nilipowahitaji.

## SHUKRANI

Naungama kuwa kazi hii haikuwa rahisi kuitekeleza lakini kupitia kwa wasimamizi wangu nimeweza kufaulu. Kujitolea kwao ni zaidi ya ilivyotarajiwa maana hawakuchoka kusoma kwa kina kazi hiyo na kunielekeza ipasavyo. Shukrani za dhati ni kwa Dkt. Omboga Zaja na Dkt. Amiri Swaleh waliyojitolea mhanga kuona kazi niliyokuwa nikiishughulikia imeafikiana kulingana na matarajio ya kozi. Urekebishaji na uelekezaji wao ulikuwa wa wazi na wa kufaa mno maaana nilipoirejelea kazi yenyewe, niliweza kuona niliyostahili kutekeleza. Nawapa kongole kwa vile waliweza kunishauri na kunielekeza ipasavyo kwani ushauri wao ulinipa nguvu na maarifa ya kushughulikia kazi yangu. Yakini usimamizi wao ulinifaa zaidi na ndiyo maana nimefaulu katika tasnifu yangu.Aidha nawashukuru wafuatao: Dkt. Iribe, Profesa Habwe na Profesa Kineene kwa maoni yao ya kutia moyo na kujitolea kwao nilipowahitaji. Ombi langu ni Rabuka awabariki kwa kazi zao nzuri.Tena sitawasahau wanakufunzi wenzangu ambao kwa pamoja tuliweza kushirikiana katika masomo ya uzamili kupitia kazi ya vikundi na mijadala tuliyojihusisha nayo kwa lengo la kudurusu kozi zetu. Ushauri wao wa kutia moyo ulinipa motisha na nguvu ya kuendelea.

## IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu ni uchanganuzi wa maswala na mambo yanayoelekea kusambaratisha na kuelekeza familia za kiafrika katika njia panda.Njia panda ina maana, waafrika wanatatizika na kushindwa kuamua iwapo wanakubali usasa au wanakubali kushikilia mambo ya jadi.Kwani licha ya maandishi haya yote ya kuwazindua wanajamii pamoja na kuzungumziwa kwa mapana kuhusu familia ya kiafrika, ni wazi bado kuna matatizo.Utafiti huu utakitwa katika *Mhanga Nafsi Yangu* ya Said A. Mohamed (2010).Riwaya hii ndiyo itakayokuwa dira na msingi wetu katika kuziweka wazi athari hizi za changamano za maisha ya sasa. Utafiti wetu umegundua kwamba,familia za kiafrika zimo katika njia panda kutokana na athari za umagharibi kama anavyoupitia Afida huko Peponi.Hata hivyo,ni wazi kuwa hata neno ‘Peponi’ limetumiwa kisitiari kuwaonya Waafrika kuwa,licha ya kwao Afrika kuitwa ‘Motoni’,kwa hakika ndiko Peponi.

## YALIYOMO

**YALIYOMO UKURASA**


**Ungamo** ........................................................................................................ii
**Kutabaruku** ........................................................................................................ iii
**Shukrani**........................................................................................................iv
**Ikisiri** ........................................................................................................v
**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI**..........................................................................1
1.0 Utangulizi..........................................................................................................1
1.1 Tatizo la utafiti......................................................................................................7
1.2 Maswali ya utafiti ...................................................................................................8
1.3 Madhumuni ya utafiti ...............................................................................................8
1.4 Sababu za kuchagua mada ..........................................................................................8
1.5. Upeo na mipaka ......................................................................................................9
1.6 Misingi ya nadharia ................................................................................................10
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada........................................................................................13
1.9 Njia za utafiti.......................................................................................................17
**SURA YA PILI: MUHTASARI NA UHALISIA KATIKA *MHANGA NAFSI YANGU***......19
2.0 Utangulizi..........................................................................................................19
2.1 Muhtasari wa *Mhanga Nafsi Yangu* ...............................................................................19
2.2 Uhalisia katika *Mhanga Nafsi Yangu* ............................................................................25
2.2.1 Usafiri ..........................................................................................................26
2.2.2 Mahusiano ya kulazimishwa.......................................................................................26
2.2.3 Kuzaa nje ya ndoa.................................................................................................27
2.2.4 Ulevi wa Afida ....................................................................................................27
2.2.5 Afida anaishiwa ...................................................................................................28
2.2.6 Uhamaji ..........................................................................................................28
2.2.7 Kutojali..........................................................................................................28
2.2.8 Tamaa ............................................................................................................29
2.2.9 Ujasiri wa Afida..................................................................................................29

2.2.10 Malezi....30
2.2.11 Mavazi....30
2.2.12 Elimu....31
2.2.13 Mfanyibiashara....31
2.2.14 Afida anaithamini na kuitumia lugha....31
2.2.15 Amejitenga na mamake....32
2.2.16 Mpishi bora....32
2.17 Hitimisho....32
**SURA YA TATU**: **USASA WA FAMILIA ZA AFRIKA**....33
3.0 Utangulizi....33
3.1 Usasa....34
3.1.1 Mahusiano ya ngono nje ya ndoa....34
3.1.2 Hali ya maisha mapya ugenini....34
3.1.3. Asasi ya ndoa na falsafa yake....35
3.1.4 Mikataba ya ndoa....35
3.1.5 Ndoa za mchanganyiko....36
3.1.6 Magonjwa....36
3.1.7 Mihadarati....37
3.1.8 Mavazi na mapambo....37
3.1.9 Vifaa vya nyumbani....38
3.1.10 Usafiri....38
3.1.11 Malezi....38
3.1.12 Hali mpya ya maisha Motoni....39
3.1.13 Muziki....39
3.1.14 Usakaji wa elimu ya kisasa....40
3.1.15 Amali za jamii kulingana na usasa....40
3.1.16 Tabia zisizoeleweka....40
3.1.17 Mawasiliano ya kisasa....40
3.1.18 Utandarithi....41
3.2 Hitimisho....41

**SURA YA NNE:ATHARI ZA USASA KWA FAMILIA ZA KIAFRIKA NA CHANGAMOTO ZINAZOIBULIWA** .......... 42
4.1 Utangulizi .......... 42
4.2 Kubadilika kwa ukubwa na muundo wa familia .......... 42
4.3 Kuibuka Familia iliyoongozwa na mwanamke .......... 43
4.4 Utengano .......... 43
4.5 Kuvunjika kwa ndoa .......... 44
4.6 Ushiriki wa wanawake kiuchumi .......... 44
4.7 Uhasama kati ya jinsia mbili .......... 45
4.8 Uhamiaji wa kimataifa .......... 45
4.9 Kubadilika kwa utamaduni .......... 46
4.10 Hali ngumu za maisha .......... 46
4.11 Migogoro .......... 46
4.12 Unyama .......... 47
4.13 Ubahili .......... 48
4.14 Kutojali .......... 48
4.15 Mabadiliko ya lugha .......... 48
4.16 Umaskini .......... 48
4.17 Maradhi .......... 48
4.17.1 Ukimwi .......... 48
4.17.2 Saratani .......... 49
4.18 Utandawazi .......... 50
4.19 Mawazo finyu .......... 50
4.20 Dawa za kulevya .......... 52
4.21 Utandarithi .......... 53
4.22 Kuwa na fikira na mawazo mapya .......... 54
4.23 Maadili mema .......... 54
4.24 Kuboreka kwa mawasiliano .......... 55
4.25 Hitimisho .......... 56

**SURA YA TANO: MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO** .................................................. 57
5.1 Utangulizi ........................................................................................................ 57
5.1.1 Kutathmini madhumuni ya utafiti ....................................................................... 57
5.1.2 Ujumla wa utafiti wetu ..................................................................................... 57
5.2 Mapendekezo ..................................................................................................... 59
**MAREJELEO** ........................................................................................................ 60

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Swala la familia ni moja ya motifu za kimsingi katika fasihi ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu familia, miungano ya kifamilia, mitagusano katika familia ni motifu za kifamilia ambazo zimeshughulikiwa na wasomi wengi. Ukweli unaoakisi mambo yanayozungumziwa katika fasihi hizo ni Katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010.Katika kifungu cha 45 inasema kuwa familia ndicho kiungo cha kimsingi cha jamii na muhimu katika kuleta utaratibu wa kijamii.Hivyo basi,katika utafiti huu tulilenga maudhui yanayohusika na familia za kiafrika ili kuulewa utaratibu huu na pia kuiboresha zaidi jamii kwa kujenga mahusiano ya mazuri katika familia kwa ajili ya kuimarisha ustawi wa jamii.Ikumbukwe kuwa kulingana na uelewa wetu,familia ni kundi la watu wanaokaa pamoja na watu wengine wenye asili moja katika uzazi wa pamoja.Kuna aina mbalimbali za familia ulimwenguni zinazohitilafiana kutokana na utamaduni na hali ya jamii.

Katika nchi nyingi za kiafrika,familia asili ya kiafrika iliweza kuonyeshwa kuwa ni baba,mama,watoto pamoja na ndugu wa baba na mama,akina babu na bibi.Kulikuwa na taratibu tofauti zilizotazamiwa kufuatwa katika mitangusano ya watu katika familia lakini ile iliyopendwa na wengi zaidi ni mume mmoja na wake wengi na kila mmoja akiwa na watoto wake.Familia ilitengemea; mila, haja ya kuafikiana na msaada wa kila mtu katika familia iliafikiwa.Ikitofautishwa na jamii za nchi zilizopita kwenye mapinduzi ya viwandani kama Ulaya na Marekani ambapo familia inamaanisha watu wanaoishi pamoja katika nyumba moja yaani baba, mama na watoto pekee.Maingiliano ya afya na usalama thabiti kwa kila mmoja ulikuwa ndio msingi wa jamii na ulifanya kila mtu katika familia za kiafrika ajisikie kuheshimiwa,mwenye furaha na salama.Mambo zaidi yaliyosisitizwa katika familia ni ukarimu,uaminifu,uhusiano mwema na wa heshima baina ya vijana na wazee.

Hali ya familia ya kiafrika imebadilika kwani kuna masuala mapya yaliyoibuka katika ulimwengu wa utandawazi kama uhamaji, ndoa za mchanganyiko, falsafa mpya za kiuhusiano wa mapenzi, hali mpya za shinikizo za kiuchumi, magonjwa, n.k. Miongoni mwa maswala ibuka kuna yale yanayoathiri familia ya kiafrika na ambayo yamezua misukosuko katika familia

hizo.Masuala haya yamesababisha mageuzi katika familia hii ya kiafrika kwani utamaduni wa kiasili unabadilika huku ukiathiri familia na hata ukileta usambaratikaji wa familia zenyewe. Kusambaratika huku kwa familia ya kiafrika ni motifu ya kimaudhui inayojitokeza katika fasihi ya Kiswahili kwani imezungumziwa kwa mitazamo mbalimbali ambapo baadhi ya wasomi wamechunguza sababu za kusambaratika kama;ulezi,utangamano,magomvi na kuathirika kwa ndoa. Usambaratikaji wa familia za kiafrika ndilo swala la kimsingi linalozungumziwa kwani ndio limechangia katika kufanya familia hizi kuwa katika njia panda na hivyo kuchanganua maswala na sababu familia za Afrika kufikia njia hii panda.

Kuna vigezo vinavyotumiwa kuangalia mitagusano katika familia za kiafrika.Haya ni maswala ya kubaguliwa katika familia, katika *Nyota ya Rehema* (1976) ya Mohamed Suleiman Mohamed, Rehema mtoto wa Fuad, anabaguliwa kwa sababu ni mweusi na haelimishwi, huku ndugu zake Samir na Salma wanaochukua rangi ya baba yao wanapewa elimu nzuri.Pia babake na mamake wa kambo (Adila) wanambagua kwa sababu ya weusi na anachagua kwenda mjini na anazama katika uasherati kuliko kutukanwa na kufedheheshwa.Ugomvi katika familia umejitokeza katika *Dunia Mti Mkavu* (1980) ya Said Ahmed Mohamed tunamwona babake Masika anamuuza bintiye kwa sababu ana tamaa ya mali ya Fauz.Tamaa ya babake Masika inabainika anapomwambia bintiye; "huoni kwamba ndoa hii itatufungulia milango ya kheri." Uk. wa 21.Ugomvi unashuhudiwa wakati Masika anabingirishana na babake,Shehe na Hamoud.Masika hamtaki Fauz na ndio maana siku ya kuingia ndani,inabidi Masika afungwe mikono na miguu ili Fauz atosheleze ashiki zake lakini baadaye Masika anamuua Fauz.Dini katika familia inaonekana katika *Nguvu ya Sala* (1995) ya K.W.Wamitila.Susan Ngunze ambaye ndiye kifungua mimba katika familia ya watoto wane:Roselyne,Jacquiline na Redempta anamwambia babake Mzee Richard,kuwa imani inayovunja familia haifai.Anawafichulia Richard na mama yake Mary Kasiva yote kuhusu kosa lao la kuifanya dini kuwakosesha mapenzi kwa watoto wao. Baada ya muda mrefu wa majibizano haya makali, Richard anaridhia na kujitolea kwenda kumrudisha Roselyne (aliyemfukuza nyumbani baada ya kufukuzwa shuleni kwa sababu ya kupata mimba) nyumbani kutoka kwa Mzee Nikodemus. Urithi unajitokeza katika riwaya ya *Kuli* (1978) ya Shafi Adam Shafi. Rashidi anarithi kazi ya babake ya ukuli kwa sababu hakupata elimu wala ujuzi. Malezi yanajitokeza katika *Tata za Asumini* (1990) kazi ya Said Ahmed Mohamed.Asumini analelewa vizuri na mamake nyumbani kwao kijiji cha Karonga.Lakini

Asumini hayafuati mafundisho na maadili hayo anapoingia Chuo kikuu kwani harudi kijijini kwao baada ya muda mfupi. *Rosa Mistika* (1971) ya E. Kezilahabi ina maswala ya kifamilia kwa namna mbalimbali,kama malezi ya mtoto wa kike,mahusiano ya ndoa,nafasi na mahali pa utamaduni wa jadi katika jamii mpya ya Tanzania,miongoni mwa mengine.

Vilevile mabadiliko haya yanajitokeza kwa kuwa umuhimu wa koo umepungua sana na mara kwa mara kuna uhuru wa mtu ndani ya ukoo kuchagua iwapo angependa kuhusiana na ndugu zake au la jambo ambalo halikuwa katika asili ya familia za kiafrika.Basi kwa sababu hiyo,kuna haja ya kuchunguza upya familia ya kiafrika ili kuonyesha jamii ilivyokuwa,jinsi ilivyo sasa,athari zilizoifanya na zinazoendelea kuisababisha kuwa ilivyo sasa, ili kuhakikisha wanafamilia wanachagua vipengele vinavyofaa katika mageuzi ambayo yanaifanya familia iwe imara na bora zaidi. Familia ya kiafrika imefafanuliwa na Kingei (1993) kuwa ni watu ambao wana uhusiano wa karibu sana kwa kuzaliwa nao, kufanya kazi nao, urafiki, ndoa, usaidizi na kuishi nao. Hapa tunapata uelewa kuwa, uhusiano ndio muhimu si lazima mtu kuzaliwa pamoja ili awe wa familia yako lakini iwapo uhusiano wowote utachangia kila wakati katika kuleta furaha, basi binadamu huyo atakuwa familia. Furaha hii itapatikana iwapo mhusika atachangia katika mahitaji ya kimsingi ya mwenzake na kujali hisia zake wakati wote kwa kuhakikisha jambo lolote analofanya, linaelekea kuleta furaha moyoni mwa mwezake.Hali hii imezua miundo mipya ya familia za kiafrika zinazotathmini namna ya kuhusiana au kuingiliana. Kwanza, kuna familia ndogo ambayo ina wazazi na watoto wao. Pili, kuna familia kubwa ambazo zina wazazi na watoto wao pamoja na wazazi wa baba na mama, ndugu za baba na mama, pamoja na watoto wao. Tatu, kuna familia ambazo mzazi mmoja tu huwalea watoto au wazazi wameachana au kutengana na wanasaidiana ulezi wa watoto. Mzazi mmoja anaweza kufa na anayebaki kuwachiwa majukumu yote ya ulezi wa watoto. Nne, zipo familia ambazo watu wazima na watoto wao kutoka katika uhusiano wa zamani uliovunjika huishi pamoja kama familia moja. Mwisho kuna familia ambayo haina wazazi, watoto wenyewe ndio husaidiana katika ulezi.

Mabadiliko haya yote katika familia asilia ya kiafrika yanadhihirisha kwa kupitia awamu mbalimbali.Kulikuwa na kipindi cha ukoloni wakati familia ya kiafrika ilikuwa chini ya himaya ya mkoloni,dini za kikristo na kiislamu ambazo ziliathiri maisha na msimamo wao.Wakoloni na wageni walivuruga hali ya shwari iliyokuwepo katika familia kwani walishirikisha familia za

kiafrika katika shughuli zao(wakoloni) kwa njia iliyowanyima nafasi za kutilia makini ukawaida wa mienendo ya maisha yao.Maadili katika jamii yalisisitizwa na yakafungamanishwa na dini ya kiislamu bila kuonyesha dini ina udhaifu ili kila mwanafamilia azingatie hulka za ubinadamu. Haya yalionyeshwa na mwandishi kama Shaaban Robert katika *Adili na Nduguze* anapoonyesha kuengemea upande wa wakoloni na kuonyesha ubora wa dini.Waandishi waliogopa kushambulia mfumo wa kikoloni waziwazi wakachangua kubaki kwenye udhahania kuliko kuukabili uhalisia moja kwa moja.

Baada ya ukoloni wa kimagharibi,wakati wa mjio wa Wamisheni ambao walisisitiza mafundisho ya familia yaliyoonyesha uhusiano baina ya mataifa ya kimagharibi na ya kiafrika.Mwarabu au Mwislamu analaumiwa kwa utumwa uliokuwemo Afrika Mashariki ilhali Mkoloni anasifiwa kwa kuleta uhuru,hata ijapokuwa utumwa ulitiliwa nguvu na ukoloni. Kwenye familia, mambo ya mila na tabia kama njia ya kufunza maadili yaliwekwa mbele hasa katika ufundishaji wa watoto.Huu pia ni wakati wa mwamko wa Mwafrika dhidi ya Mkoloni, wakati wa mwafrika kuanza kuupata utaalamu wa kusoma na kuandika na akaanza kupata na kushuhudia tajriba za kitaaluma na kifalsafa za kigeni.Maudhui ya udhalilishaji wa Mwafrika yaliyotokana na fasihi ya kimagharibi kama katika *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi* ilioandikwa na Gerishon Ngugi. Naye Shaaban *Robert* aliandika kuhusu matarajio ya familia itakikanayo baada ya ukoloni katika *Siku ya Watenzi Wote*. Maudhui kuhusu maisha na mapenzi yalihusishwa.

Hivyo, kipindi baada ya miaka kumi ya uhuru, katika jamii miongoni mwa familia chache kulionekana na ulundikaji wa mali na ukandamizwaji wa familia nyingi. Vilevile uhuru wa kisiasa,unafiki,ukoloni mamboleo,ufisadi,usaliti wa umma,ujamaa,utawala wa kiimla ulikithiri katika familia ya kiafrika. Katika kazi ya Shaaban Robert,*Utubora Mkulima* mhusika mkuu Utubora anafunga nikaha na Radhia na wanakuwa na familia ambayo inaonyesha maadili ya kufuatwa katika jamii na hasa kutoka kwa Utubora mwenyewe kama, adabu njema,unyenyekevu na ufasaha wa maneno na vitendo. Imani inayotokana na dini ya kiislamu kujenga familia imara na kutazama mbele miaka mingi ijayo.Uhuru ulizifanya baadhi ya familia za kiafrika zitamani kukurubiana na jamii, hasa wanafamilia walipotanabahi kwamba elimu yao imewakengeusha.Baada ya mwaka wa 1978 mpaka sasa, uhusiano katika familia huru ya

kiafrika, mvutano baina ya utamaduni wa kisasa na wa kale na maana ya maisha ya sasa ni athari zinazoletwa na urithi wa ukoloni kwa jamii na kwa watu binafsi.

Kutoelewana kumeifikia kila familia ya kiafrika ambako kunafikiriwa ni kwa sababu ya mageuzi, hivyo basi  kuhitaji msaada  ili kueleza kwa nini kuna kutoelewana huku.Katika tasnifu yetu tulilenga kubaini na kudhihirisha kwa nini hali ya mambo iko jinsi ilivyo na kuonyesha jinsi familia hizi zimebadilika kwani swala la mageuzi lingaliko na litaendelea kuweko.Hali hii ya mageuzi haya huchochewa na changamoto ambazo huathiri hali ya mahusiano  katika familia ya kiafrika. Kwa sababu hii, pia tulionyesha na kuthibitisha changamoto za usasa, usomi na uigaji wa tamaduni mpya/za kigeni zinazoibuliwa na mabadiliko katika familia ya kiafrika. Dhana ya usasa kwa mwelekeo wa fasihi hutumiwa kuelezea mielekeo mipya ya kitamaduni na kisanaa iliyoibuka hasa baada ya Vita Vikuu vya pili vya Dunia vilivyoanza mwaka wa 1939 na kufikia tamati mwaka wa 1945 (Suakei 2013:13).Anaendelea kusema ni vigumu kuweka wazi mpaka baina ya ukale, usasa na usasaleo kwani kila mhakiki huwa na mwono tofauti na mwingine kuhusu dhana hizi. Usasa huu unaweza kujitokeza katika tungo za fasihi kuonyesha vile mambo haya ya kisasa yanavyotagusana na binadamu na kumsibu na kumwathiri kwa hali chanya au hasi. Pili, ni Usomi na utamanduni wa kigeni. Mitagusano na wageni hawa inazidi kuvuruga utaratibu wa mifumo ya elimu ambayo ilikuwako kabla. Elimu ya kimagharibi imeleta mambo mapya na hata kuvurunga thamani pamoja na maadili katika jamii. Maadili yanapovurungika uhusiano unaathirika katika familia kwani kuna wale wanaodhibiti maadili ya asili na wale wanaoiga utamaduni wa wageni.

Ni muhimu kutaja kuwa kuna vipengele vilivyo na athari ya juujuu katika mahusiano ya familia, kama: watu wanaomzunguka mtu kama marafiki au watu wanaozunguka ndio wanaoweza kuwa chanzo cha kuibua utofauti, kwani maneno wanayoyasema katika kujadili mambo yanaweza yakawa ni sumu kali na yenye kuibua matatizo katika jamii. Hivyo kubomoa au kujenga baadhi ya maingiliano katika familia.Ni muhimu usuli wa maisha ya mtu binafsi ndio chanzo cha jinsi mtu anajiona katika nafsi yake na ndivyo ulivyo na ndivyo watu watakavyokuona.Usuli huu unaweza kumpa mtu swali la kujiuliza jinsi ajionavyo nafsini mwake na ndilo litakalokuwa chimbuko la kuibua furaha au huzuni maishani mwake,iwapo mtu ana furaha maishani

itadhihirika katika maingiliano yake,ikiwa ana huzuni atakuwa mwenye kusikitisha katika mahusiano yake na ya kifamilia .

Usasa ambao ndicho kitovu cha athari zinazoikumba familia ya kiafrika umeshughulikiwa na Suakei (2013). Ametafiti dhana ya usasa kama inavyoakisiwa katika kazi za kisasa za kifasihi kwa kumsawiri, kumzungumzia na kumwasilisha mwanamke wa kisasa.Ameshughulikia *Nyuso za Mwanamke* ya S.A. Mohamed na kuziweka wazi nyuso za mwanamke kwa mtazamo wa usasa akiongozwa na nadharia ya ufeministi wa kiafrika.Vilevile kuna mawazo yasiyo ya kiusomi katika mtandao hasa katika mitandao ya kijamii ambayo yanazungumzia usasa kwa ufinyu kwa mfano kuna wale wanaotumia mada zifuatazo, athari za kutumia teknolojia ya sasa,mavazi ya kisasa ambayo hayafai,namna ya kuhusiana vyema katika ndoa za kisasa,matatizo ya mahusiano ya ndoa ya kisasa. Pamoja na uelewa huu anuwai katika kazi hii bunifu, tunapata taswira ya familia iliyo katika njia panda kutokana na kuathirika kwa aina ya mitagusano ya kifamilia na changamano za maisha ya sasa.Uhakiki wa kazi hii umeziba pengo lililopo kuhusiana na suala la familia ya kiafrika kwani ni kipindi cha kufanya maamuzi muhimu ya maisha na hivyo, hili ni swala muhimu sana katika uhakiki wa fasihi.

Tulilenga kubainisha na kudhihirisha mambo yanayohusisha mazingira ya kifamilia katika riwaya teule ya Said A.Mohamed. Huyu ndiye mwandishi wa riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*, alizaliwa Pemba, tarehe 12 Dicemba mwaka wa 1947. Alizuka kwenye ulingo wa fasihi kwa hadithi fupi zake zilizotangazwa kwenye idhaa ya Kiswahili ya BBC kuanzia miaka ya sabini na kuchapishwa baadaye. Aliwahi kufunza vyuo vingi katikaAfrika Mashariki vikiwemo Chuo Kikuu cha Moi (Eldoret) na Chuo Kikuu cha Nairobi kabla ya kuteuliwa Profesa katika Chuo Kikuu cha Osaka, Japan.Baadaye aliendа kufunza katika Chuo Kikuu cha Bayreuth nchini Ujerumani.Ni mwandishi mwenye kipawa cha aina yake katika uandishi wa riwaya.Riwaya zake zingine ni pamoja *na Asali Chungu* (1977),*Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Kiza katika Nuru* (1988) *,Tata za Asumini* (1990), *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006), *Nyuso za Mwanamke* (2010), *Mkamandume na Mhanga Nafsi Yangu* (2012) ambayo ndiyo tuliyoishughulikia.

Kwa ufupi, kazi yetu ilichunguza mambo yafuatayo:
Uhalisia na usasa wa familia za kiafrika, athari za usasa zinazoikumba familia ya kiafrika, changamoto zinazoibuliwa na athari za usasa na mwisho, kukadiria familia za kiafrika zinaelekea wapi?

## 1.1 Tatizo la utafiti

Tatizo la utafiti tuliloshughulikia ni uchanganuzi wa maswala na mambo yanayoelekea kusambaratisha na kuelekeza familia za kiafrika katika njia panda.Kwa maana, waafrika wanatatizika na kushindwa kuamua iwapo wameukubali usasa au wamekubali kushikilia mambo ya jadi.Kwani licha ya maandishi haya yote kuwazindua wanajamii pamoja na kuzungumziwa kwa mapana kuhusu familia ya kiafrika ni wazi bado kuna matatizo.

Utafiti huu ulikitwa katika *Mhanga Nafsi Yangu* ya Said A. Mohamed *(2010)* na ndiyo iliyokuwa dira na msingi wetu katika kuziweka wazi athari hizi za uchangamano wa maisha ya sasa.Mwandishi huyu amedhihirisha athari za usasa zinazoikumba familia ya kiafrika kwani ndizo zimesawiriwa kupitia mhusika mkuu Afida, anayeikimbia nchi yake ya Motoni na watu wake kwenda kuishi na kutafuta riziki yake Peponi.Anahajiri na kuishi Peponi kwa sababu kwao hakuna maisha yoyote ya maana.Safari ya Afida ni ya matumaini lakini matumaini yanapigwa teke na uchangamano wa maisha yake mapya mara tu anapofika Peponi.Maisha yake mapya yanatawaliwa na usasa na usasa huu unaathiri mahusiano kati yake na familia yake.Kwa mfano, shangazi yake Bi.Marneti aliyemfanyia wema wa kumleta Peponi ndiye anayekuwa adui yake.Vilevile ahadi za Afida kuusaidia ukoo zinavunjwa na mahusiano mema yanakatikakatika.
Lengo kuu la kazi yetu lilikuwa ni kufafanua kwa kuyaweka wazi mawazo mazito yanayoikumba jamii ya kiafrika ya sasa, kama yanavyojitokeza katika riwaya hii na kubainisha jinsi mwandishi huyu anayajadili maswala haya ya familia na hasa katika kuonyesha changamano za usasa zinavyoathiri familia za kiafrika. Aidha tulionyesha kuwa riwaya hii tuliyoishughulikia katika tasnifu hii imesawiri familia ya Afrika kwa namna tofauti ambayo imetufungua macho kama jamii kuona mambo yaliyo asilia.

### 1.2 Maswali ya utafiti

Maswali yafuatayo ndiyo yaliyotuongoza katika utafiti wetu:

a) Mwandishi ameshughulikia vipi maswala ya uhalisia na usasa katika familia za kiafrika?

b) Je, ni maswala gani mwandishi wa *Mhanga Nafsi Yangu* anayoyapa kipaumbele?

c) Je, ni changamoto zipi zinazoibuliwa na maswala ya usasa na zinazoathiri familia za kiafrika?

### 1.3 Madhumuni ya utafiti

Tulidhamiria kuchambua na kuchanganua *Mhanga Nafsi Yangu* kimaudhui ili:

i. Kubainisha jinsi mwandishi alivyoshughulikia uhalisia na usasa wa familia za kiafrika.

ii. Kudhihirisha maswala yanayopewa kipaumbele katika riwaya teule.

iii. Kuchunguza na kufafanua kwa kina changamoto zinazoibuliwa na athari za usasa kwa familia ya/za kiafrika.

### 1.4 Sababu za kuchagua mada

Uteuzi wa mada hii umeshawishiwa na mambo kadha wa kadha. Kwanza,ni kuitazama jamii kwa jumla badala ya kuitazama kama familia ya kiafrika kwa kushughulikiwa katika mitazamo ya kijumla ambapo riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* inaweza kutumiwa kama kielelezo kwani unapoisoma unapata kwamba suala linalotawala ni uhusiano katika familia.Mhusika mkuu ana matumaini maishani baada ya kupata "bahati"ya kwenda Peponi.Lakini bahati hii inazua utangamano mpya wa maisha unaoambatana na matatizo mengi kwa mhusika mkuu.Matatizo hayo ni yale yanayomkumba binadamu yeyote katika maisha.Pia utafiti huu ulilenga kuwahamasisha wasomaji wa fasihi wajikite zaidi kulenga masuala ya familia ambayo ndicho kitovu cha afya ya maisha.Muhimu zaidi ni kuwa suala la athari za changamano za usasa zinavyoathiri familia linamhusu kila mwanadamu wa kike au kiume na hivyo, lazima uhusiano mwema udumishwe ndipo kila mja aweze kuishi kwa amani na mwenzake.Basi ni vyema wanafasihi wajumuike pamoja katika kuagazia swala la familia za kiafrika.

Sababu ya pili,ilihusiana na haja ya kutaka kuelewa kama nafasi ya utandawazi na uhamaji ni kuzikuza au kuzisambaratisha familia .Sababu ya tatu ni kuichanganua riwaya hii kwa misingi ya uhalisia ili kuweza kuonyesha jinsi mwandishi wa riwaya hii anavyotoa tahadhari juu ya changamoto za usasa zinazoathiri familia za kiafrika za kisasa.Nne,Shirika la Umoja wa Mataifa lililoundwa mwaka wa 1945 huko San Francisco, Marekani, limekuwa msingi mzuri wa kisheria

katika uhusiano wa kimataifa.Umoja wa mataifa, kupitia vyombo vya sheria na taasisi za ushirikiano na misaada kama vile shirika la umoja wa mataifa linaloshughulikia mradi wa chakula ulimwenguni, shirika la elimu, sayansi na utamaduni, liliandaa mipango madhubuti ya kueleza, kushauri na hata kuyaadhibu mataifa yatakayotatiza amani duniani.

Msingi wa amani hii ni uelewa wa jinsi watu wanavyohusiana katika shughuli zao za kila siku hasa katika familia kwa sababu uhusiano katika familia, umejikita katika usambazaji wa maadili ya uvumilivu,heshima na haki miongoni mwa jamii za ulimwengu.Hivyo basi, maadili haya husambazwa katika mataifa ya ulimwengu.Kuwepo kwa katiba ya Umoja wa Mataifa ni mafanikio makubwa.Hii ina umuhimu wa pekee wa kihistoria na ni rasilimali ambayo haina gharama yoyote kwa utu na ubinadamu.Kuwepo kwa katiba hiyo ya Umoja wa Mataifa ni jambo la kufurahia.Kuadhimishwa kwa miaka 50 ya mkataba huo wa Umoja wa Mataifa ulikuwa tukio muhimu kwani kuna hali ya baadaye isiyotabirika iliyotokea kwa hivyo,mawazo yaliyomo katika mkataba huo wa umoja wa Mataifa yanabidi yapewe msukumo mpya.Uwezo wa kukabili changamoto mpya unabidi uimarishwe.kuwepo kwa kanuni za mkataba huo wa Umoja wa Mataifa unataka kila kizazi kipya kiahidi upya kuwajibika kwake katika kudumisha umoja na mshikamo wa binadamu duniani. Ni kwa mujibu huu ambapo tulidhamiria kuhakiki athari ya changamano za usasa katika *Mhanga Nafsi Yangu* kwani ni muhimu amani idumishwe na iwepo katika familia na hivyo kuchangia katika ufanisi wa jamii kwa jumla.

Kwa misingi hii tulitarajia kwamba utafiti wetu utaliziba pengo hili na utakua daraja madhubuti ambalo watafiti wa baadaye watavukia ili wajadili tanzu zingine za fasihi ambazo tulifungia nje kwa sababu ya ukosefu wa wakati wa kutosha.

**1.5. Upeo na mipaka**

Utafiti huu ulishughulikia maudhui ya changamoto za usasa,na jinsi zinavyoathiri na kuweka familia za kiafrika katika njia panda. Maswala haya yalishughulikiwa katika *Mhanga Nafsi Yangu* kwa misingi ya mkabala wa kiuhalisia. Pamoja na kutambua kuwa mwandishi wa riwaya hii ametumia ujuzi mwingi kama vile kuwasilisha kazi yake kiujozi. Swala hili la kiujozi hatukulishughulikia kwani malengo yetu ya kimsingi yalijikita katika maudhui, bila ya kujingiza

katika mtindo, iwapo yalitajwa, basi yalihusiana moja kwa moja na jinsi yalivyofanikisha maudhui haya katika kazi hii.

Hatukujikita katika vipengele vilivyomhusu mwandishi kama vile tabaka lake, jinsia yake, matamanio yake wala kujikita katika uchapishaji na usambazaji wa vitabu vyake,bali tulijikita katika kutathmini kipengele cha jinsi utandawazi ulivyoathiri familia ya kiafrika.

## 1.6 **Misingi ya nadharia**

Utafiti huu ulifanywa kwa kutumia msingi wa nadharia ya uhalisia.Uhalisia kama chombo cha kuchanganua na kutathmini watunzi lilianza kudhihirika kuanzia mwaka wa 1800 nyakati za mwandishi wa kifaransa Gustar Flaubert.Nayo dhana ya uhalisia, ilianza kujitokeza zamani sana katika kipindi cha enzi za kati, yaani baina ya 1100-1500 baada ya Kristo. Ilipitia mabadaliko mengi ya kimatumizi kama yalivyofanywa na wataalamu kama vile Emmanuel Kant (1790) na hata Schiller (1798).Nadharia hii iliwekewa msingi na Hegel (1979) katika kitabu chake kinachojulikana kama *Introduction to Aesthetics.* Mtaalamu huyu alipendekeza matumizi ya neno ‘uhalisia’ kuelezea kazi ya kifasihi ambayo inawasilisha ulimwengu na maisha ya jamii ambako kuna mhusika anayetenda mambo kwa jinsi inayochochewa waziwazi na hali aliyomo. Msingi mkubwa wa nadharia hii ni usimulizi wa kimuhakati. Huu ni usimulizi ambao unasimulia matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi au kwa namna inayokaribiana sana na hali iliyoko katika jamii.

Nao Boyle na Swales (1986:107) wanasema kuwa mwandishi Proust, alitaka kuandika juu ya kile kingeonyesha umuhimu wa nafsi na aliyoyapitia kwani mwandishi wa kazi ya uhalisia inampasa azungumze mambo jinsi yalivyo katika jamii yake. Msingi mkubwa wa nadharia hii ni usimulizi wa kimuhakati.Huu ni usimulizi ambao unasimulia matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi au kwa namna inayokaribiana sana na hali iliyoko katika jamii. Uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya kijamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Mtazamo huu unatilia mkazo kwenye uwasilishi wa mambo ambayo yanaonekana wazi katika jamii.

Kulingana na Msolike (1993:106), uhalisia ulianza mwaka wa 1820 B.M. Kishikilizi cha nadharia hii ni wazo kuwa, sanaa inafaradhiwa iseme ukweli, iwe aminifu na ionyeshe hali hizo waziwazi.Ni aina ya mtazamo wa kifasihi unaochukulia kazi za kifasihi kama zinazoakisi sifa za

kimsingi zinazohusishwa na uhalisi yaani hali halisi za maisha katika jamii husika.Naye Mbatia (2001:92) anasema uhalisia ni tapo la uandishi uliozuka Ulaya katika karne ya kumi na nane na kusambaa katika mataifa mengine ya ulimwengu. Baadaye anaendelea kusema kuwa wasanii wa kiuhalisia walijishughulisha kuutafuta na kuubainisha ukweli wa maisha ya kila siku ya mwanadamu. Hivyo basi Said A.Mohamed anasawiri jinsi maisha ya familia yalivyo katika mazingira halisi ya jamii.

Mbatiah (2001;92) anasema kuwa uhalisia ulizuka katika bara Ulaya katika karne ya kumi na nane na kusambaa katika mataifa mengine ya ulimwengu na wasanii wa uhalisia walijishughulisha kuutafuta na kuubainisha ukweli wa maisha.Waliamini kuwa ukweli huo uliweza kupatikana katika maisha ya kila siku ya mwanadamu.Walisawiri mazingira halisi ya jamii kama ilivyo.

Wamitila (2002:115-116) anaeleza kuwa wanauhalisia hujifunga kwenye wahusika wa kawaida au wanaoweza kupatikana katika jamii halisi,huyachunguza na kuyasimulia maisha yao na tajriba zao,husawiri na kuonyesha mandhari na mazingira ya kawaida wakati wa kuandika kazi zao. Mwandishi kwa hivyo anapaswa kuyaakisi maisha ya jamii katika ngazi ya kijamii, kiuchumi, kitamaduni na kisiasa. Uhalisia unatilia mkazo uwasilishaji wa mambo ambayo yanaonekana katika jamii na anayeandika kwenye msingi wa tapo hili basi anatilia mkazo wahusika katika hali za kawaida za maisha, matukio na mandhari ya kawaida kama yanavyojitokeza katika jamii.

Ntarangwi (2004) anasema nadharia hii humaanisha uwakilishi wa uhalisi wa mambo katika fasihi,na ilizuka katika karne ya kumi na tisa hususan kupinga ulimbwende.Mwanauhalisia huamini ukweli unaozingatiwa ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajriba.Hivyo uhalisia huwa katika mambo yaliyopo ya matukio halisi kwa matokeo yanayoweza kuthibitika. Imani ya mhalisia ni kwamba kazi ya fasihi yapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida,wa kweli na halisi.Hivyo basi hata picha za ulimwengu atakazoumba msanii,zapaswa kudhihirisha hali hiyo.Mhakiki anayezingatia nadharia hii ya uhalisia hupembua namna mtunzi alivyodhihirisha uhalisi wa mambo kupitia maudhui aliyoyazingatia na wahusika aliowasawiri.

Hivyo tulionyesha jinsi ukweli ulivyodhihirishwa katika juhudi za mtunzi kuchora hali halisi ya mambo katika wakati maalum.Kwa muhtasari basi msanii anatarajiwa kusawiri wahusika,matukio na mandhari yanayokubalika na kuaminika katika jamii ya wakati wake.Ufahamu wa mazingira na maisha anayoyalenga mtunzi ni nguzo muhimu kwa mhakiki wa kihalisia.

Wafula na Njogu (2007:63) wanasema uhalisia unahusishwa na kipindi maalum cha kihistoria katika jamii za Ulaya. Kilianza mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa nchini Ufaransa na kilihusishwa na waandishi Balzac, Stendhal na Flaubert. Hawa walisisitiza maelezo ya ‘kikweli’ katika kazi zao na waliamini kuwa dhima ya mwandishi ni kuonyesha ukweli jinsi ulivyo. Uhalisia ulienea katika nchi nyingine za ulimwengu kutokana na mapinduzi haya yaliyosababisha kuzuka kwa mambo mapya katika nyaja mbalimbali za maisha mfano, upanuzi wa miji.Matatizo yaliyofanana na mambo hayo ndiyo yaliyowafanya waandishi wengi kuudhihaki ulimbwende na kuanza kuandika juu ya hali halisi ya maisha ya jamii. Hapa ndipo wanatilia mkazo kwa kusema kuwa mwandishi anapaswa kuitoa picha ya jamii bila kuidunisha wala kuipigia chuku. Anaendelea kusema kulingana na Wamitila (2003:272).Mtaalamu mwingine anayehusishwa na uhalisia ni mfuasi wa Marx kutoka Hungary anayejulikana kama George Lukacs.George Lukacs anasema uhalisia ni lengo kuu la msanii na zaidi mwandishi (katika kuandika) anapaswa kusukumwa na nia ya kuusawiri uhalisi katika wakati fulani maalum.Hivyo basi inadhihirisha kwamba, uhalisia unapingana aina yoyote ya majaribio.Vilevile, wanaeleza dhana ya uhalisia ilianza kutumika takribani mnamo mwaka wa 1790. Katika mwaka huo, Emmanuel Kant katika chapisho lake lililoitwa *Critique of Judgment* aliitumia istilahi ya udhahania kamilifu kama kinyume cha uhalisia. Katika mwaka wa 1798, wahakiki kama vile Sehiller walikuwa wakitumia maneno haya yaani udhanifu na uhalisia kuashiria kinyume. Dhana ya uhalisia imekuja kuhusishwa na miktadha miwili kwanza inatumiwa kama njia ya kutathmini hali au halia yaani uhalisia wa maisha na kifasihi. Kwa sababu hii tuliashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha kwani maoni haya yanahusiana na kazi tuliyoishughulikia *Mhanga Nafsi Yangu* kwani inahusu mhusika mkuu Afinda na aliyoyapitia, katika maisha yake.

John (2011) katika tasnifu ya Karoki (2014) anasema kuwa, mwanzo wa kutumia mtindo wa uandishi wa kiuhalisia ulitokana na Honore` de Balzac, mwandishi na riwaya na tamthilia wa Ufaransa (1799-1850). Anaendelea kusema kuwa uhalisia katika fasihi sana sana unahusishwa na mwamko wa kimaandishi uliotokea Ufaransa katika karne ya 19. Aina hii ya uandishi inahusishwa mno na mwandishi wa riwaya Flaubert (1821-1880) kutoka Ufaransa. Anachukuliwa kuwa mmoja wa mihimili ya uhalisia. Josh pia anasema kuwa Howells William Dean (1837-1920) ndiye mwasisi wa uhalisia Marekani.

Nadharia hii ilitufaa katika utafiti huu ikizingatiwa kuwa maswala ambayo mwandishi anayaangazia kuhusu familia yanaendelea kumkumba binadamu kote ulimwenguni na hasa Afrika katika karne hii ya ishirini na moja.Tuliitumia kama msingi wa uchunguzi wa riwaya teule kwani mambo yanayojitokeza katika *Mhanga Nafsi Yangu* ni ya kweli na vilevile ni mambo tunayokumbana nayo katika hali halisi ya maisha yetu ya kila siku.

Pamoja na hayo vipengele vya uhalisia tulivyotumia ni: Kwanza, usawiri na uelezaji wa hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha kwa maana ya uigaji wa mazingira anayopatikana mwanadamu. Kipengele cha pili ni ukadiriaji wa uhalisi wa maisha katika maandishi ya mtunzi.Tatu ni uangaziaji wa mshikamano uliopo kati ya maelezo ya kubuniwa na uhalisi wa maisha kama tunavyoyaelewa.Nne,kwa kujikita katika vipengele hivi vitatu tulitumaini kuonyesha jinsi masimulizi ya kiubunifu katika *Mhanga Nafsi Yangu* yanarandana katika maisha halisi ya jamii ya mtunzi hasa kwa jamii za kiafrika kwa jumla.

### 1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Muda mwingi wa utafiti huu ulikuwa kupitia maandishi kwa madhumuni ya ukusanyaji data.Kuna mengi yaliyoandikwa juu ya uhalisia,jamii kwa jumla na familia ya kiafrika.Scott (1972:3) katika kitabu chake,ameeleza maana ya uhamiaji,hali ya uhamiaji na kuangazia uhamiaji wa watu kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu,Marekani.Kitabu hiki kimetusaidia kupata maana ya uhamiaji,athari kutoka tamaduni mpya na changamano zilizopo katika uhusiano katika maisha baada ya uhamaji.Hii ni kwa sababu Marekani ni sawa na Peponi katika *Mhanga Nafsi Yangu* kwani kama Marekani Peponi kunachukuliwa na wa Motoni kama mahali pa bahati na uzuri wote wa maisha na hivyo kila mmoja kupata mshawasha wa kuhamia huko.

Mcneill na Adams (1978:337) wameeleza maana ya uhamaji,shida za uhamaji na manufaa yake.Maandishi yao yameingiliana sana na kazi yetu kwa sababu shida hizi baadhi zinatokana na uchangamano wa maisha ya sasa na hivyo zinatupa mwongozo kwani ndizo zinaathiri mahusiano katika familia.

Marquez (1980) si mwasisi wa uandishi wa kisasaleo isipokuwa anafikiriwa na wasomaji wengi kuwa mwandishi wa kifantasia.Kwa mfano, Wamitila anaona hali ya wahusika wanaopatikana kwenye riwaya ya Marquez, *One Hundred Years of Solitude* ambao wanaishi chumba na choo bila kutambua kama mambo yaliyokiuka uhalisia. Kinyume na madai haya, yeye mwenyewe (Marquez) amedai mara nyingi kuwa ni mhalisia ambaye anajaribu kuelezea jinsi hali ilivyo nchini mwake Kolombia kwa njia ya kweli iwezekanavyo. Williams naye anasema kuwa, Marquez anaelezea kuhusu wafanyakazi wa Macondo ambao wanaandaa mgomo. Baadaye uvumi unaenezwa kwamba serikali imewaua mamia ya wafanyakazi. Kisa hiki kimetajwa kuwa cha kifantasia kuliko vingine lakini kwa maoni yetu ni uhalisia kwa sababu wanatafuta haki wapo katika mandhari yao ya uhalisia ambayo ni Macondo na kisa chenyewe kina mihimili ya nadharia ya uhalisia.

Senkoro (1982) amepiga hatua ya kuieleza lugha kama kipengele muhimu zaidi katika fasihi kwani ndicho kinachotofautisha fasihi na sanaa nyinginezo.Lugha basi,ndiyo njia ambayo mwanafasihi hutumia kuyaeleza mambo yanayohusu jamii yake kwa ubunifu na kiusanii.Ukweli wa kauli ya Senkoro unadhihirika katika *Mhanga Nafsi Yangu* kwa sababu mwandishi ametumia lugha kwa njia ya kiubunifu ili kuwasilisha ujumbe kama tulivyoona.

Sarara (1997) ameshughulikia kazi za Said Ahmed Mohamed kwa kujishughulisha na matatizo yanayotokea katika jamii.Anasema chanzo cha matatizo hayo ni ubepari na lengo la sasa ni kuzua harakati za kuibadilisha hali na kujenga jamii mpya inayotarajiwa kutokana na mageuzi hayo.Ameshughulikia tamthilia za *Pungwa* (1988),*Kivuli Kinaishi* (1990) na *Amezidi* (1995) za S.A.Mohamed.Nasi tulishughulikia jamii lakini kwa undani au kiunzi chake ambayo ni familia ya kiafrika.Tofauti naye,sisi tulihakiki riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ili kuonyesha jinsi mitagusano katika familia za kiafrika imeathirika pia,uelewa na mwono-ulimwengu wa msanii

katika kazi hii, jinsi mawazo yake yanavyoibuka katika mchakato wa athari za changamano za usasa. Jinsi kuaminika huku kumefungamanishwa na ukunjufu wa uelezwaji wa familia za Afrika mpya.Huku kulituwezesha kubainika kwa uhalisia na kuaminika kwa maongezi na matendo ya wahusika;mambo ambayo hatimaye, yalitusaidia kutathmini changamoto zinazoibuliwa na athari zinazoikumba familia ya sasa ya Afrika.Tulifanya hivi kama njia ya kuweka misingi mwafaka tuliyoitumia hatimaye kupima na kutathmini matapo makuu ya familia kwa ujumla, maudhui makuu ya mwandishi yanayojitokeza katika riwaya tuliyochagua katika misingi na imani kwamba swala la familia ya Afrika yameshughulikiwa kwa wakati ufaao.

Gromov(2002:3-4) ameeleza kuwa usasaleo ni njia ya kuufinyanga ukweli wa maisha kwa njia tofauti na jinsi ilivyozowewa .Kulingana naye uhalisiaajabu ni kitengo cha usasaleo ambacho kimefanikiwa kuzungumzia maswala ya kileo nasi katika utafiti wetu tulishughulikia maswala haya ya usasaleo katika kuonyesha usasa wa familia za kiafrika.

Walibora (2010:147) ameshughulikia maswala haya ya usasa kwani anasema kuwa, maoni ya Khamis (2005) na yale Williams katika kitabu chake *Marxism and literature* (1999) yanashabihiana ambapo Williams anasema kwamba mikakati ya kimajaribio katika sanaa hudhamiria kuakisi ukosefu wa uthabiti katika michakato ya kijamii. Aidha, kuibuka kwa riwaya za usasaleo kulibadili hali iliyokuweko hata zaidi (Williams 1995:1). Walibora (2010:143-157) vilevile ameshughulikia uhalisia katika *The Tin Drum* (1965) na *Dunia Yao* (2006), na kwa kujua au kwa kutojua waandishi hawa wawili wamo katika 'dayolojia' ambayo twaweza kuifasili kama mawasiliano au mazungumzo yanayowezesha kuigana na kuathiriana kimtindo na kimaudhui. Kimsingi, fasihi moja inasema au inajibizana na nyingine au kutoa mwangwi wa mambo yanayofanana au kulingana na yale ya fasihi nyingine. Kutokana na maelezo hayo tunapata kuelewa kuwa Walibora anaonyesha hali halisi katika vitabu hivyo vyake viwili.

Wanjiru (2013) amechunguza vipengele vya uhalisia na uhalisiaajabu vinavyodhihirika katika riwaya za Said Ahmed Mohammed, *Babu Alipofufuka* (2002) na Tom Olali Babu,*Watu wa Gehenna( 2012)* Ameonyesha ni kwa nini uhalisiajabu ni njia mwafaka zaidi ya kusoma na kuzifahamu riwaya hizi mbili. Wameta kuwa waandishi hawa wametumia lugha yenye ubunifu mwingi, uhusika usiozoeleka na mandhari ya kiajabu kusawiri kazi zao.Uandishi wa aina hii

unahitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina ili kubainisha mwelekeo wa waandishi hawa. Kuna pengo kati ya yale tunayoyajua katika uhalisia na yale ambayo hatuyaelewi katika ndoto lakini yanaonekana kama mambo halisi.Ameushughulisha uhalisia sehemu unapojitokeza tu.

Katika tasnifu yake,kwa kuchunguza mandhari na wahusika katika kazi zote hizi,anasema uhalisia ni muhimu sana katika maisha ya binadamu.Naye Said Ahmed Mohammed katika riwaya yake ya hivi karibuni ya *Nyuso za mwanamke* (2010), anarudia uandishi wake wa uhalisia akiangazia wanawake waliofanikiwa hata ikiwa wanakumbana na changamoto nyingi zikiwemo masuala ibuka, yenye migogoro mingi ya kumdunisha mwanamke.

Kulingana na Caleb (2013:8) akimnukuu Sutherland (1957) amesema, "jinsi ambavyo mwandishi alivyoandika hutegemea kipindi alichoandika, tabaka alimozaliwa, elimu aliyopata pamoja na dini yake".Kauli hii ya Sutherland itatufaa kwa kuwa, kazi ya mwandishi aghalabu huangazia masuala yanayoikumba jamii ya mtunzi katika kipindi husika. Maelezo yao yanaingiliana na kazi yetu kwa njia sawa kwa kuwa jambo hili linadhihirika katika *Mhanga Nafsi Yangu* kwani masuala anayoyaangazia mwandishi kuhusu familia, yanajitokeza katika karne hii zaidi ya vile ilivyokuwa katika karne zilizopita.
Suakei (2013:51) ameueleza usasa kuwa,

> "Kuendelea kwa binadamu kulingana na jinsi ulimwengu ulivyo kunatengemea anavyowaza, anavyoshughulikia ulimwengu na bidii aliyo nayo ya kwenda sambamba nulimwengu unavyosonga mbele."

Ameweka wazi suala la mwanamke wa kisasa kwa kuonyesha vile mwanamke wa kisasa anavyopambana na usasa kwa kutumia vigezo vya kisasa.Kazi hii imetusadia kwa sababu tunajishughulisha na suala la usasa lakini kwa kuchunguza jinsi uchangamano wake katika maisha ulivyoathiri mitagusano katika jamii.

Mtaalamu mwingine ambaye alitufaa sana katika utafiti wetu ni Karoki (2014) amesema mwandishi George Eliot alianzisha nadharia ya uhalisia Uingereza nao Mark Twain na William Dean Howells wakawa waasisi wa uhalisia Marekani. Karoki amesisitiza kuwa Uhalisia hujishughulisha moja kwa moja na kile kinachotekwa na akili kwani mwandishi Mwingereza-

Mmarekani, Henry James alikuwa mmoja wa wana-uhalisia maarufu sana na alipata mvuto huu uliotuvuta sisi vilevile kwani akili zetu zinatekwa na kuathirika kwa mahusiano ya jamii na usasa. Usasa ni ule unaoakisi maendeleo ya jamii ya sasa katika nyanja mbalimbali kama utangamano baina wanajamii,elimu,siasa,uchumi,teknolojia,mavazi,biashara,lugha na majilio ya utamaduni wa kigeni.Usasa huu unafasiriwa kuhusiana na nyakati za sasa,za hivi majuzi au hivi karibuni na zenye sifa zinazohusiana na usasa kulingana na mitazamo ya jamii,fikra zao,na maendeleo yao kwa jumla. Ni maelezo muhimu kwani yanazungumzia nadharia ya uhalisia ambayo ndio msingi wa utafiti wetu.

Vilevile katika utafiti tulionyesha fafanuzi kadha wa kadha za familia katika riwaya teule, kwa misingi ya kijumla na katika misingi ya fasihi ya Kiswahili. Hii ni kwa nia ya kuonyesha wajibu, majukumu na mahusiko ya mitagusano katika kuibusha familia ya kisasa .Vilevile tulichunguza changamano za usasa zilizotumiwa kumulika na kusawiri ukuaji wa mawazo katika misingi ya nafasi na majukumu ya wahusika katika riwaya hii na jinsi nafasi zao zilivyoweza kutumiwa kama msingi wa kutathmini ukuaji wa familia ya kiafrika ya kisasa na hata kukua kiuchangamano kwa riwaya ya Kiswahili na fasihi ya Kiswahili kwa ujumla.

### 1.9 Njia za utafiti

Tulisoma vitabu, tasnifu, majarida na machapisho yaliyoandikwa na waandishi mbalimbali ili kumudu kabisa mada yetu ya utafiti. Tulisoma kazi teule katika misingi ya nadharia ya uhalisia, kisha tukafuta data ambazo zilijumuisha maelezo, fafanuzi, mifano,ndipo tukapata ithibati na ushahidi wa kuimarisha mijadala na madai tuliyoyatoa katika utafiti wetu. Lengo la usomaji huu lilikuwa ni kutafuta data zilizohusiana na ufafanuzi wa mada tuliyoishughulikia katika msingi wa nadharia tuliyoitumia katika utafiti. Data tulizotumia ni zile zilizohusiana na familia na kama zilivyofafanuliwa na wataalamu mbalimbali katika fasihi ya Kiswahili.

Kwa kuwa *Mhanga Nafsi Yangu* inashughulikia maswala yanayohusiana na athari za usasa zinazoikumba familia na ndipo nadharia ya uhalisia ikasadifu kwa utafiti huu. Tumedhamiria kuchota data za upili ambazo zitahusu mitagusano, maingiliano ya kifamilia, athari za usasa zinazoikumba familia ya kiafrika na changamoto zinazoibuliwa na athari za usasa. Tumezichambua data hizo katika misingi ya uhalisia ili ndipo hatimaye tukafikia mahitimisho

juu ya mambo hayo na yanavyochangia katika kuathiri na kuziweka familia za kiafrika katika njia panda.

Vilevile tumetumia mtandao kwa lengo la kutafuta marejeleo ya ziada kuhusiana na changamano za usasa na malengo ya usasa kadri zinavyoathiri au jinsi zinavyoathiri familia za kiafrika .Vilevile tumetafuta marejeleo zaidi kuhusu mada yetu na nadharia ambayo tunaitumia ndipo tukapata mwelekeo bora zaidi katika utafiti wetu.Tumehusisha maoni ya wataalamu wa fasihi na nadharia na kuwahusisha wasimamizi wetu na wasomi wengine katika mijadala.Haya yote yamechangia katika kufanikisha utafiti wetu huu.

## SURA YA PILI

## MUHTASARI NA UHALISIA KATIKA *MHANGA NAFSI YANGU*

### 2.0 Utangulizi

Sura hii inaeleza muhtasari wa riwaya teule ya *Mhanga Nafsi Yangu*.Umetolewa ili kuwepo na uelewa wa kazi iliyojadiliwa na kumpa mwanga mtu yeyote atakayeitalii kazi hii.Vilevile, uhalisia wa familia za kiafrika kama unanavyojitokeza katika *Mhanga Nafsi Yangu* umejadiliwa kwa kuangalia aina za maingiliano ya uhalisia wa familia za kiafrika.

### 2.1 Muhtasari wa *Mhanga Nafsi Yangu*

Hadithi inaanza Afida akiwa ndani ya *AirUropa* akielekea Peponi.Ana mawazo mengi sana ambayo yanamfunga kuitawaza furaha. Furaha anayopaswa kuwa nayo kwani amepata bahati njema ya kwenda Peponi. Kwenye mawazo ya Afida tunarudi nyuma katika mwagano na ukoo wake mkubwa katika uwanja wa ndege wa kimataifa. Afida anaeleza kuhusu mshikamano wa ukoo unavyozidi kuangamiza kwa kuwa Waafrika lazima wagawane mafanikio yote. Katika mwagano Afida anatoa ahadi kwa; Bi. Zaina, Bi.Sinangoa, Bi. Mwamda (mamake), Kisura na jamaa zake wote wanakuwa na matumaini naye.Vilevile akiwa ndani ya Air Uropa,anajisaili kuzaliwa mtoto wa kike, na kuhusu sababu ya wageni wengi kuondoka makwao kuja Motoni.Babake Afida Bwana Daudi, anajitokeza ndotoni ya Afida na hamwitikii wala hataki kumkumbatia Afida kama alivyofanya zamani alipoona babake yu tayari kuondoka kwa safari ya muda mrefu.Kwenye ndoto Afida anakumbuka mafunzo ya mwalimu wake,uhusiano wake na babake katika utoto wake. Baadaye Afida anagutuka kutoka kwenye ndoto, anapata ndege ikiwemo katika hatua ya kuteremka katika uwanja wa ndege wa Peponi,na anagundua kila kitu ni cheupe Peponi.

Ukurasa mpya wa maisha ya Afida Peponi unaanza. Ni majira ya baridi Peponi na hawezi kulala kwani baridi ilipenya kila kipembe na kumwingia hadi mifupani kila siku.Yuko ndani ya kujichumba kidogo anamolala ambamo hamkuwa na vukuto la joto la kutosha, huku shangazi yake Bi. Marneti na mumewe Bwana Bawa wakiishi kwenye chumba kikubwa kilichojaa uvuguvugu na raha.Tunaona nyumbani kwa Bi. Marneti kumejaa samani na vifaa vya haja ya

usaidizi wa binadamu. Afida anakumbuka mwalimu wake wa somo la siasa alivyowahi kuwaonya shuleni juu ya utashi wa vitu.Alisema utashi wa vitu ni haja na fahari ndiyo unaambatana na balaa. Afida aliona tu ni choyo ya kukosa kumiliki vifaa hivyo.

Tunaangaziwa mwezi mmoja tu baada ya Afida kufika Peponi anapomsikia shangaziye Bi. Marneti na mumewe wakigombana.Bw.Bawa anasisitiza lazima alazwe kwenye chumba chenye joto la kutosha kwani si uungwana kumlaza kwenye chumba kile chenye baridi ya kumtia mtu maradhi, naye Bi. Marneti anasisitiza alazwe huko azoee baridi na ndivyo ilivyo sasa. Asubuhi anaamka na kitetemeshi, cha mwili na mafua Bi. Marneti anampeleka hospitali na njiani anamwonya kutotazama kwa mfululizo macho ya Mwani kwani yana mvuto wa ajabu. Zahanatini Bi.Marneti anadanganya daktari kuwa Afida analala kwenye chumba chenye vuguvugu la kutosha.Baadaye Afida anatukumbusha kuwa anakatazwa na Bi. Marneti kukoga kila siku kwani Peponi hakuna joto kama Motoni, na hata akikoga mara milioni kutwa moja hatakuwa mweupe kama wapeponi. Siku hii Afida akinyatianyatia kwenda kukoga anasikia ugomvi baina ya Bi. Marneti na Bw.Bawa. Bwana Bawa alisema Bi.Marneti alimwonea wivu Afida ambaye ni mwanaye na mtoto wa dadake. Bi.Marneti anakana wivu na kueleza kuwa alitaka Afida apelekwe shule akasome.Wanadhihirisha kuwa maisha yao yameharibika tokea kuja kwa Afida.

Baada ya kukoga Afida yuko chumbani mwake, hana kitu au mtu wa kusema naye na hivyo basi anaanza kusema na sauti.Alisema kuhusu kukerwa na masusuiko ya Bi. Marneti nayo sauti ilizungumza kuhusu wenye pesa ambao hununua vitu kwa mchezo tu, si kwa haja na wale wanaoweza kuhasiri roho za watu wasio na hatia kupata wanachotaka.Vitu hivi ndivyo vilivyobadilisha upya mawazo ya Afida.Afida anatuonyesha maisha ya Bi. Marneti yalivyokuwa akiwa Motoni alikuwa hana ugomvi, alipenda mapenzi safi na vilevile mwenye kuchangua maneno ikitofautishwa sasa alivyo mgomvi na mwenye kupenda watu walio mbali yaani Wapeponi. Tunapelekwa mbele siku ambayo Afida amesimama peke yake kwenye kituo cha basi. Ni majira ya baridi na amejifunika maguo mazito mazito mwili mzima.Amegundua mambo kuhusu Wapeponi; kila kitu kinaendeshwa kwga wakati, Jumapili si siku nzuri ya kutoka, kwani ndio siku wapeponi hupumzika na kujifungia ndani ya majumba yao. Yeye ametoka kwani amechoka kuketi ndani na kukerwa na nafsi yake, anataka kuzururazurura nje. Akingoja basi

anamkumbuka mwalimu wake wa fasihi, Mzee Dawamu alivyowasaidia kuchambua shairi la majira ya baridi Peponi. Ingawa awali alikana shairi lile sasa anaona mawazo yake ni ya uhakika na kamilifu.Ndani ya basi anaketi na kuingia ndotoni, anakumbuka Motoni msimu wa kipupwe wakati kuna mboga na matunda ya kila aina. Ndipo maskini husimamisha vimeza na vigari vibovu kando mwa barabara kuuza matunda ili kukusanya faida chache za kulisha koo zao kubwa. Hawa pia ndio hupigwa picha sana na watalii.

Miezi tisa inapita na watu wengi katika ukoo wa Afida wamemwandikia barua na kumuuliza hali na kumkumbusha wajibu wake. Amewajibu wachache tu, tena kwa nadra,na hivyo wamekasirika na kusema kwenye barua kuwa yeye ni msaliti wa ukoo. Anapukutikwa na machozi akikumbuka ladha tamu ya mapenzi yake na Shaabani yanavyozidi kufifia. Zaidi ni kuwa watu wa ukoo wanaagizia vitu wakati yeye mpaka sasa hana uwezo wa kununua kitu chochote zaidi ya mahitaji yake ya kila siku na pesa ni za kugawiwa.Basi linasimama kwenye kituo kimoja mbele na Shuhuda rafiki yake anaingia. Shuhuda ana uzuri wa kuvutia, alivalia kipeponi na kutenda kama Wapeponi. Afida anashawishiwa na Shuhuda kufanya (kutenda) kama Wapeponi lakini anaghairi. Afida anatueleza hapendi watu wanaofuga nywele kirasta, na anaturudisha nyuma siku ya kwanza kumwona Saparata. Saparata ni mtukutu, anayesomea tamaduni za kiafrika katika Chuo Kikuu cha Peponi. Saparata humfuata Afida kila mahali akimtamani lakini hapumbaziki. Shuhuda na Afida wakati huu wanakaribishwa na Saparata kwenye sehemu ya mapumziko ‘Zaman’ na kununuliwa vinywaji naye. Hapa Afida anapokea simu kutoka kwa Shaabani anayemwarifu amelezwa hospitali katika chumba mahututi kutokana na maradhi ya moyo.Ujumbe huu unasababisha Afida kubogoja kitini lakini anadakwa na Shuhuda. Shuhuda na Saparata wanampeleka nyumbani kisha siku mbili baadaye anaelezwa kifo cha Shaabani na kwa miezi mitatu hakuweza kunyanyuka kitandani kwa huzuni. Bi. Marneti alikasirika sana na kumtishia kumrudisha Motoni. Anakarambuka na Bi. Marneti anamwondosha kabisakabisa nyumbani na kumpeleka chuoni kusoma kipeponi.

Mienzi tisa inapita, Afida anaeleza shida za pale Taasisi ya Lugha ya Peponi. Tokea siku ya kwanza wenzake darasani wanamtenga, wengine wanambagua, naye mwalimu wa darasa hakumwamini kabisa kama angeweza kuwa na akili ya kufahamu kipeponi na pia pesa za matumizi alizoletewa na Bi. Marneti hazikutosha kamwe. Anahitimu masomo ya miezi tisa ya

lugha ya Peponi,na kupokea zawadi ya kuwa mwanafunzi wa kwanza wa Motoni kufaulu vizuri tokea miaka kumi na tano iliyopita.Usiku wa manane bwenini Chuo Kikuu cha Peponi, mwaka mzima umepita.Afida yuko kitandani anagaragara, usingizi hauji na hawezi kumudu masomo yake pia. Sauti zinaanza kupenya ndani ya ubongo wake, kumtaka adadisi usiku na mchana wa Motoni. Siku hizi anachukia sauti zile zinazomrejesha Motoni bila ya kusita kwani alishafika pahala alipopatamani siku nyingi. Anajisemea kuwa watu wa kwao mpaka sasa huwajui hana chochote anachokichuma mwenyewe, nategemea pesa za kugaiwa tu. Sauti inasema Motoni ni pahala pa balaa tupu kisha Afida anaeleza tafsiri ya usasa ambao unaimarika na kubadilika kwa namna nyingine katika kipimo cha nukta na dakika. Kila wakati akili yake inamwambia ana haki ya kudharau maisha ya Motoni. Anakumbuka maisha yake yote, anakumbuka jinsi babake alivyokuwa ruwaza kwake;kila Alhamisi kuamkia Ijumaa yeye pamoja na watoto wa nyumbani,wa majirani na wa mitaani walivyokusanywa na babake akawasikiliza jinsi walivyoendelea kumudu kitabu kitakatifu.Vilevile udogoni alivyowafundisha Abjadi na alivyofurahia kusoma,hasa jinsi angerekebisha historia ya ubinadamu katika siku zijazo.

Babake Afida anatiririkia chumbani kupitia dirisha kwa mzunguko wa *sufism*, akimfanya Afida kushangaa kwani miaka miwili hajaja kumzuru.Babake kwanza anamkumbusha nasaha alizompa,za kutenda na kutendana, kutenda na kutotenda. Pili dini zote zinaelekea Aheri na hakuna atakayekuwa anamjua mwenzake katika familia yao. Tatu mahubiri aliyowapa ni ukweli mtupu wa maisha na mwishoni anamfafanulia na kumwonyesha utengano wa Afida na mamake na yeye Afida hakuwa na furaha kama zamani. Mazungumzo haya yanamfanya Afida kujitathmini, anapatwa na huzuni na kuputikwa na machozi. Babake anapoondoka anapatwa na usingizi.

Afida anatueleza kuhusu uhusiano wake na Yakrobich. Anakutana na Yakrobich wanapofika wiki moja kabla ya kuanza masomo ukumbini mwa *Leisure Hall* katika Taasisi ya Lugha Peponi anapovutiwa na muziki.Yakrobich anamnunulia chakula na soda, wanafahamiana na kucheza densi pamoja hasa wimbo wa Marvin Gay *What's going on*? Uhusiano wao sasa umekua zaidi ya miaka miwili isipokuwa Afida anakataa mapenzi ya mwili naye kwani haoni kama yatamletea furaha. Yakrobich ni limbukeni wa Peponi Mashariki,mtoto wa matajiri wapya, mwenye heshima na mshindani asiyependa kushindwa.Afida anatukumbusha babake aliyekuwa kiongozi

harakati zote za dini alivyomdokezea kuhusu *Sufism*, umuhimu wa muziki kwa mwanadamu akimwelekea muumba wake na alivyompa uhuru usiokuwa na mipaka hadi akawa shabiki wa muziki nyumbani na mitaa ya karibu na kwao.

Maisha yanamregeza na kuubaradhulisha ushujaa wa Afida hadi anaubadilisha msimamo wake. Neshboch, mzee wa miaka sitini na miwili na mpenda maisha anamgundua Afida nyumbani kwa shangaziye na kwa sababu hii anafanya sherehe nyingi nyumbani kwake ili kumteka Afida lakini anaambulia patupu, kwani kila wakati anamnyemelea kwa namma jeuri na ya kumdhalilisha. Bw. Bawa na Bi. Marneti wanamshawishi kumkubali na siku moja Afida anamkubalia usuhuba tu. Neshboch anamtembeza kwenye utajiri wake na wanakula na kunywa kwa utonofu.Yakrobich anapongundua Afida ameimili upande wa Neshboch, anapandwa na hasira na kumwambia anajiuza na kuwaibisha vijana wote hivyo anajenga ukuta wa dharau na chuki kati yao.Bi. Marneti anayejua uhusiano wake na Yakrobich anambakulia Afida kuwa Yakrobich si rafiki bali anataka kumkandamiza tu, anamtweza Neshboch kuwa mwenye busara na faida kuliko Yakrobich kwani anaweza kumpatia uraia.Mwanga wa uhitaji wa mtu kama Neshboch unaanza kumwingia Afida na nasaha za Bi. Marneti zinamwingia nafsini, anajisabilia kwa Neshboch kabla ya ndoa kukamilika, wanapata mtoto nje ya ndoa hadi uzito huu wa mambo unamfanya Afida kuahirisha masomo kwa miaka tatu. Neshboch anampatia Afida msaada anaouhitaji katika maisha yake na ya mtoto na kulipiga chenga suala la kufunga ndoa mwanzoni lakini mwishowe anakubali na wanafanya harusi.

Mfululizo wa majira unaleta kero badala ya furaha Peponi kwani mwanzoni maisha ya ndoa na Neshboch yanakuwa murua kabisa anatawazwa umalkia, pesa na neema zinamzunguka naye Dinda mtoto wao wa kiume anacheza naye na kuzungumza kuhusu maisha. Uhusiano wa Bi. Marneti na Afida unaanza kuwa mzuri anapohakikishiwa na Afida kwamba kwa vyovyote asingeingia mikononi mwa mumewe, lakini anapozaa tu! Uhusiano wao unachafuka tena anapomshawishi Neshboch na kubali kumpa mtoto wao wamlee kwani huwa tasa lakini Afida haruhusu hilo.Maovu yanazidi She-shaiza (ndugu ya Neshboch) anapoamua kumuandama kwa simango za ubaguzi.Miaka minane imepita na ndoa ya Neshboch na Afida imeshuhudia mabadiliko mengi kwani haina mashiko ya mapenzi ya kweli kwa sababu waliifunga kwa kigezo cha utajiri na uzawa wa Neshboch Peponi.Siku hii Afida anaeleza kuwa ameshapata uraia na

paspoti ya Peponi na She-shaiza anakuwa mtu wa kwanza kumkejeli.Ukejeli huu unamfanya Neshboch na BendelheiB waingilie kati lakini Neshboch anatetea She-shaiza,jambo linalomfanya Afida akasirike,kutoka nje na kuchukua gari,na kulitimua bila ya kumsubiri Neshboch.Anaenda kwa Profesa Marjan na mkewe Mama Maryam wanaompa mawaidha kusimama kidete na kuwaonyesha Neshboch na She-shaiza udhaifu wao kwa njia ya uungwana.Vilevile wanamfahamisha kuwa Shuhuda alikuwa amelazwa hospitalini kwa ugonjwa wa kisasa usiopona.Siku baadaye Neshboch anampiga Afida nusura amuue kama Dinda asingeingilia na baadaye anamfungia nje. Nje anawapigia Profesa Marjan na mkewe simu ili waje kumchukua na jioni ile, ndoa yao na Neshboch inafikia kikomo. Profesa Marjan na mkewe Mama Maryam ni baba na mama wa kupanga wa Afida, wanatoka nchi moja jirani ya Motoni. Afida anakutana na Profesa Marjan Chuo Kikuu cha Peponi kwani ndiye Profesa wa mwanzo kutoka Motoni kuja kusomesha Peponi. Hawa wanamchukua kama mtoto wao, wanampa nasaha na fikra za kijituuzima. Afida anapewa talaka na kufukuzwa na Neshboch bila chochote.Mahakama inampa haki ya kukitunza kitoto chake na vilevile inaamuru Neshboch amtafutie Afida pahala pa kuishi na Dinda, na kudhamini gharama za kuendesha maisha ya Dinda; jambo ambalo linamkera Neshboch mno.

Siku moja usiku polisi wanapigiwa simu na majirani wa Afida na kuambiwa kwamba Afida ana mchezo wa kurudi usiku wa manane katika hali ya ulevi ‘topu’ na anapoingia ndani amezoea kukipiga makofi ki-Dinda.Jambo hili si kweli kama polisi wanavyopekua.Lakini mahakamani hakimu anambandika jina la ‘mama katili’ huku wakili wake Afida akinunuliwa kwani haitetei kesi ya Afida kihalali. Afida analemewa jinsi mahakama inavyomkandamiza na kumwangusha chini kwa kumpa haki mumewe. Suala la Neshboch kumpiga vibaya vibaya Afida hadi anakaribia kufa, linageuzwa na kumfanya Afida kuwa ndiye mkosa kwa vile anamghadhabisha Neshboch kupita kiasi.

Haruhusiwi kukilea kitoto chake Dinda kwa kisingizio kwamba ni Mama mlevi. Katika unyonge wa kutengwa na ki-Dinda, Afida anapoteza kabisa imani anayokuwa nayo kuhusu Peponi na pia kuupoteza mwili wake ambao hapo zamani alidhani ungekuwa wake wa kumsabilia mwanamme mmoja tu ambaye anampenda na kumheshimu, zaidi anashindwa kuzuia tabia ya kunywa pombe kwa wingi, anaingia katika mtego wa kukaribishwa ulevi na wanaume kwa mtindo wa nipe

nikupe. Afida anakuwa hatoki tena kwenye baa akiwafuata wafadhili wake ambao nao wanataka kufadhiliwa. Babake anapomzuru na kumkaripia kwa kuyaharibu maisha yake, anamfukuza na kumwita maiti asiyejua chochote.Baadaye anapasua kilio,analia kwa uchungu na kuwaza kwa nini alimkubalia Neshboch kunywa pombe na kumpa mimba. Anajiwa na fikra ya kupata mtoto mwingine na anapokuwa katika baa maarufu ya 'The Lost'anakutana na Saparato; wanakunywa pombe mpaka wanakuwa hawajitambui tena na kulala kitanda kimoja nyumbani kwa Saparato. Kitoto kinachozaliwa kinaitwa Mkombozi.

Kuzaliwa kwa Mkombozi kunamfanya Afida aache ulevi moja kwa moja kwani sheria ya Peponi isingeruhusu mama mlevi aachwe alee mtoto. Anapewa pesa na serikali kumhudumia mtoto, lakini hazitoshi kwa hivyo anatumia ufundi wake wa kuchonga vinyago na kufuma vitambaa vya mapambo na kuviuza. Pesa anazozipata anazitumia kama nyongeza ya zile anazopewa na serikali kumhudumia Mkombozi. Siku moja anapokuwa akichonga kinyago anapata maumivu makali tumboni. Anaenda hospitali na kugunduliwa na saratani ya fuko la uzazi, anafanyiwa operasheni.Siku moja baadaye anapokuwa amelazwa hospitali (baada ya kufanyiwa operesheni) anajiwa na mwuuguzi wa wadi ya UKIMWI anayemwomba afike kwenye wadi kumwona Shuhuda aliye katika hatua yake ya mwisho.Afida anaenda, wanazungumza na Shuhuda hadi anaishiwa na nguvu.

Miezi sita baada ya kifo cha Shuhuda, Profesa Marjan anapokea simu kutoka kwa Afida akilia kwa gugumio na huzuni, anasema; anaumia kwa nini mamake hakumuua wakati alipomzaa, mamake aambiwe amsamehe na amwombee kwa babake anapomtilia ubani,na mwisho anaomba asamehewe na Profesa Marjan na Mama Maryam kwani dunia imemfikisha pabaya kisha akakata mawasiliano.Profesa anapoenda kumfuata hampati kamwe, anamwona Mkombozi pekee, anamchukua na kumwacha ndani ya mikono ya polisi. Miaka sita imepita na Profesa Marjan hajakutana na Afida na hakuna anayemwona wala kujua alikokwenda.

### 2.2 Uhalisia katika *Mhanga Nafsi Yangu*

Katika sehemu hii tulionyesha masuala halisia kama yalivyojitokeza katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* kwa sababu yaliyoelezwa ni ya kweli kwani ni kioo cha hali halisia ilivyo katika familia ya kiafrika ya kiafrika. Vilevile tunamuunga mkono Mbatiah (2001:92)

anayesema,wanauhalisia walijishughulisha kuutafuta na kuubainisha ukweli wa maisha.Waliamini kuwa ukweli huo uliweza kupatikana katika maisha ya kila siku ya mwanadamu.Kwa hivyo walijikita katika mazingira halisi ya jamii na kujaribu kuyasawiri kama yalivyo bila kupotosha,hivyo basi katika sehemu hii tumeionyesha hali halisi ya familia za kiafrika kwa kutumia riwaya hii kama dira yetu.

### 2.2.1 Usafiri

Kwa sababu ya hali mpya za shinikizo za kiuchumi, wanawake wamekuwa viumbe vya kiuchumi kukimu nafsi zao na familia zao hii ndio sababu Afida anapopata mwaliko kutoka kwa shangazi yake Bi.Marmneti kwenda Peponi,anaiona hii kama bahati na kusafiri kwenda Peponi.Uhitaji wa familia yake unaonekana wakati ukoo wake ambao ndio familia yake,unapojitolea vilivyo kwa kuja naye katika uwanja wa ndege wa kimataifa kumwaga,kumpa maagizo na kila mmoja kumweleza mahitaji yake ambayo yeye Afida anapaswa kutekeleza afikapo Peponi. Kwa mfano,Bi.Sinangoa alitaka atengenezewe safari kwenda Peponi kupata matibabu ya tumbo,Bi.Zaina alitaka tiketi ya kwenda Peponi kutia meno na pia Afida amletee dola mia tano ili kutia bati nyumba yake ili kumvuta bwana mpya,naye mamake Afida,Bi.Mwamda alitaka anunuliwe gari moja kubwa la kubeba mizigo na basi moja la kufanyia biashara ya kupakia abiria,(uk. 7).

Hii ni ithibati tosha kuwa Afida alikuwa ni chombo cha kukimu mahitaji ya familia yao na hivyo kukoleza huhitaji wake wa kuchukua safari hii.Haya yote ni kwa sababu wamepata mawazo mapya ya kiuchumi na kijamii juu ya haki za binadamu.

### 2.2.2 Mahusiano ya kulazimishwa

Ukoo wa Afida unamwandikia barua mfufulizo akiwa Peponi na kumkumbusha wajibu wake. Lakini yeye anawajibu wachache tena kwa nadra.Kwa sababu hiyo wanakasirika kama walivyoonyesha ndani ya barua zao,(uk. 67)Wanajaribu kulazimisha uhusiano wa karibu na Afida na kusisitiza ndani ya barua zao mara kadha alipe fadhila.Hata hali ya kuandika barua mfululizo, bila wengine wao kujibiwa na kuzidi kuandika tena na tena ni kulazimisha Afida kuhusiana nao bila yeye kutaka.

Saparata analazimisha kuhusiana na Afida kama inavyojitokeza, Saparata anampigia Afida simu mfululizo mpaka Afida anasema,

> “Siku zote nilipozisikiliza zilikuwa zinanata uchimvi.Kwa namna fulani simu zake zilikuwa kero kubwa kwangu na uke wangu…Nilijaribu kuzipuuza simu zake.Tatizo ni kwamba hajui kukata tamaa.”

Zaidi kila wakati alidai apewe fursa amchukue usiku kumtembeza lakini Afida anakataa kila wakati na kumpa dharura ya kuwa alikuwa akisoma, (uk. 91).

### 2.2.3 Kuzaa nje ya ndoa

Afida anapata mtoto nje ya ndoa wakiwa na Neshboch kutokana na kujisabilia kwa Neshboch kabla ndoa yao haijarasimika,(uk. 146).Hali hii inahimarisha uhusiano wake na Neshboch kwani Neshboch hamkatai mtoto wake Dinda bali anamchukua kwa hali na mali.Baadaye Afida anapopoteza ki-Dinda ndipo anapopoteza moyo wake na anapogundua ukweli huu akielekea katika baa ya “the lost” anapata jawabu au uono mpya, na anaamua kupata mtoto mwingine nje ya ndoa kwa sababu tayari ndoa yao na Neshboch imekamilika.Anapatana na Saparato kwenye “the lost” anamkubalia uhusiano wa mapenzi siku hiyo na baadaye anapata mtoto wa pili aitwaye Mkombozi.

### 2.2.4 Ulevi wa Afida

Afida anaanza kulewa kutokana na uhusiano wake na Neshboch anayemsisitizia kwa kumshikilia na kumhamakia kila siku kuwa akinywa pombe ataona raha,ikambidi aonje kidogo;na anapokwisha kuonja kidogo ikawa kidogo na kidogo tena,na tena na tena mpaka anakuwa mlevi mwenye udhia kabisakabisa,(ukurasa 178).Katika unyonge wa kutengwa na ki-Dinda, Afida anapoteza kabisa imani yake kuhusu Peponi, anashindwa kuzuia tabia ya kunywa pombe kwa wingi, anaingia katika mtego wa kukaribishwa ulevi na wanaume kwa mtindo wa nipe nikupe. Afida anakuwa hatoki tena kwenye baa kuwafuata wafadhili wake ambao nao wanataka kufadhiliwa.Ata katika baa maarufu ya ‘*The Lost*’anapopatana na Saparato;wanakunywa pombe mpaka wanakuwa hawajitambui tena na kulala kitanda kimoja nyumbani kwa Saparato,(uk 177-183).

### 2.2.5 Afida anaishiwa

Kutokana na Afida kushiriki ulevi,sasa hana pesa kwani ulevi umemkaushia pesa,(uk 176).Hii ni kwa sababu Neshboch hana jukumu tena la kumlipa pesa za kukihudumia ki-Dinda kwani amemnyanganywa haki ya kukilea na mahakama kwa kisingizio cha mama katili anayehatarisha maisha ya ki-Dinda kwa ulevi topu.Hata baadaye pesa anazopewa na serikali kuhudumia Mkombozi hazikutosha hata alizopata kwa kuuza mapambo zilitosha kama nyongeza ya kumhudumia Mkombozi tu.(Ukurasa 185)

### 2.2.6 Uhamaji

Afida anahama kutoka kwao Motoni alikozaliwa na kukulia na kwenda Peponi kwa shinikizo la kiuchumi ili kukimu ukoo wao na kusaka elimu.Peponi analazwa kijichumba kidogo ambamo hamkuwa na vukuto la joto la kutosha mbali na chumba kikubwa cha Bi.Marneti,shangazi yake na mumewe Bwana bawa kilichojaa uvuguvugu na raha.Baada ya kupatwa na mafua anahamishwa na kupelekwa chumba karibu na wanacholala wao,ambacho kina mitambo ya joto inayofanya kazi vizuri.Afida anahamishwa nyumbani kwa shangaziye na kupelekwa Chuokikuu cha Peponi kusoma Kipeponi.Anahamishwa kutoka chuoni na Neshboch na kwenda kuishi naye jumba lake la kifahari baada ya kupata mtoto Dinda .Baada ya ndoa yao na Neshboch kusabaratika mahakama inaamuamuru Neshboch amtafutie Afida pahala pa kuishi na hicho kitoto chao na hivyo anahamia katika mojawapo ya *flats* za Neshboch katika ukurasa wa 172.Anahama hapo baada ya kupokonywa malezi ya mwanawe Dinda na kuishi katika ulevi kwa kulala na wanaume kiholela ili wamfadhili kwani hana pesa.

Baada ya kujifungua mwanawe Mkombozi anaiacha tabia hii na wanaishi naye,hapa ndipo baadaye anapotokomea asionekane tena.

### 2.2.7 Kutojali

Afida amefikia hali ambapo hajali kuvuja sheria za Peponi na hajali nafsi yake kama anavyomwelezea mwenye baa ya ‘*The Lost*

> “Niitie hata kundi la polisi na majeshi, nitasema, nitasema tu…” (Uk. 181)

Hapa alielezwa anyamaze lakini hakusikia badala yake anayaweka wazi matendo mabaya anayofanya kwani babake anapomzuru na kumkaripia kwa kuyaharibu maisha yake hivyo Afida anamfukuza na kumbwatia kuwa hakujua chochote kuhusu maisha, (uk 177).

Afida anaonyesha kutojali ahadi alizoipa familia yao kabla ya kwenda Peponi.Hii ni kwa sababu anapoandikiwa barua na kuulizwa hali na kukumbushwa wajibu wake anawajibu wachache tu, tena kwa nadra sana hata hakuzitimiza ahadi alizowapa,(uk 67). Jambo hili linaonyesha baadaye familia yao ikikasirika, kwani hasira hizi wanazionyesha ndani ya barua zao zinazotaja waziwazi kuwa yeye ni msaliti wa ukoo, kwa kusahau ahadi alizowapa walipokuja kumuaga katika kiwanja cha ndege. Wanasisitiza ndani ya barua zao mara kadha kuwa Afida hajui kulipa fadhila. Afida hajali kwani anasema hata hakumbuki namna walivyomfunza alipokuwa kinyando.

### 2.2.8 Tamaa

Tamaa ya vitu inazidi kumjaa Afida moyoni mwake na inamzidi nguvu,hana kizuizi nayo kwa ule mshawasha wake,katika ukurasa wa 92.
Tamaa inamfanya kuzungumza na Saparata bila ya kupumbazika kwa kumkubalia kikao naye, wanapopatana gafla tu Afida anakubali kula naye kwa nia ya kutimiziwa haja yake ya kulipiwa bili.Saparata anamlipia Afida bili ndogo na kubwa na Afida anaona si vibaya watu kuwa na ushirikiano wa aina hii tu, kwani jambo hili linathibitisha uhakika katika dunia hii ngumu. Anamtumia Saparata tu!Kukithi uchu wake wa vitu, (uk. 85).Mkolezo wa idhibati tosha wa tamaa hii unajitokeza babake Afida anapomwonya Afida anavyogeuka bila ya kujiona wala kujitambua kuwa mtu mwingine kwa kuwa ana utashi wa vitu na pupa ya pesa, (uk 93).Hajali wale wote wanaompenda kwa kutotimiza ahadi alizopeana na kwa sababu ya tama hii,

> “Pesa baadaye hazikutosha kamwe, kwani hazikuzima tamaa ya vitu vilivyozidi kujaa moyoni mwa Afida. Tamaa ya vitu sasa inamzidi nguvu” (uk 92).

### 2.2.9 Ujasiri wa Afida

Afida anapoingia shule anajieleza mawazo yake bila soni (si mpole kama awali) haya yanajitokeza anapokuwa darasani kwani anasikiliza kila kitu kwa makini, anasema bila kujali makosa, bila kuona haya au aibu, anauliza anapokosa kujua na anajibu inapombidi ajibu,(uk 90).

### 2.2.10 Malezi

Wazazi ndio wanaojenga msingi wa tabia ya mtoto lakini Afida ameasi malezi aliyopewa kwani amebadilika na babake anapomweleza kubadilika huku anamkemea kwa kumwambia wako katika dunia tofauti nay eye amejaa ukale.

Afida anawaona Profesa Marjan na mama Maryam kama wazazi wake kuliko Bi.Marneti ambaye ni shangazi yake.Uono huu unatoka na sababu kuwa kuna maingiliano ya kifamilia kati ya Profesa Marjan,mkewe mama Maryam na Afida kwa kuwa Profesa Marjan na mkewe wakiwa Peponi, wanakuwa wazazi kamili,wanamchukua Afida kama mtoto wao,na kumpa nasaha na fikra za kijituuzima. Mama Maryam anathibitisha uhusiano wa kifamilia kwa Afida kwani Afida anapomwarifu amepata ujauzito wa pembeni na kwa hivyo ingembidi aache chuo kikuu kwa muda, Maryam anajawa na uchungu wa mwana na mama mzazi,na machozi yanamtoka na hata anataka kumsaidia kumlea mwanawe Afida hadi awe mkubwa haya ni katika ukurasa wa 158.Maingiliano yao ni ya karibu sana hivi kwamba wanamshughulikia Afida hadi anapopotea na hata mienzi sita baadaye wanazidi kumtafuta kwa usaidizi wa polisi,huu ni ulezi asilia.

### 2.2.11 Mavazi

Mavazi ni sehemu ya utamaduni wetu kwani binadamu huvaa mavazi tofauti kulingana na hali na pia kama njia ya kuonyesha heshima kwa utamaduni wa jamii,wazazi na jamii. Asili ya mavazi haya ni kulingana na tamaduni ambazo ni lazima kufuatwa na kila mmoja kwenye familia za jamii husika.Katika familia za Motoni inakuwa ni jukumu la kila mzazi katika familia yake kuakikisha kuwa mavazi ya mwana wao ni yale yamekubaliwa na jamii. Zaidi wazazi wote yaani baba na mama wanahusika kuhakikisha haya yametekelezwa, ndio maana si mamake Afida pekee anayehusika katika kumweleza Afida namna atakavyovalia anapobaleghe,Darweshi babake Afida anakuwa katika mstari wa mbele kumpa mawaidha na kumwonya namna ya kuvalia.Anamwambia kujifunika mtandio au kanga tokea kichwani mpaka kifuani, avae kanzu mbwangambwaga isiyoonyesha mkatiko wa mwili wake. Na katika umri wa ugori anahimizwa avae buibui ambalo linamfunika mwili mzima isipokuwa usoni, (Uk 74). Tokea ukiwa mtoto unalelewa kwa kunyooshwa na kulazimishwa kuvaa kama jamii nzima inavyovaa bila kupewa nafasi ya kufanya unavyotaka.

Hii ndio sehemu ya mtagusano kati ya Shuhuda na Afida ambao wanapingana anapokuwa anasoma lugha ya Peponi kwani Shuhuda anamsihi Afida kuvaa kisasa kama yeye anavyovaa lakini Afida anakataa na kuendelea kuvaa kitamaduni. Lakini sasa Afida anavalia tofauti na alivyovaa Motoni kwani uk. 165 anatueleza mavazi mapya aliyonunuliwa na Neshboch.

> "Vivazi vya nje na ndani vya bei kubwa katika maduka ya feshini vilirundikana kwenye makabati.Viatu vya kila aina vilipangana kwa mlolongo mrefu."

### 2.2.12 Elimu

Afida anapopata ujauzito nje ya ndoa inambidi aache masomo yake Chuo kikuu kwa muda ili kumlea mwanawe hadi awe mkubwa, (uk. 158). Hata baadaye haendelei na masomo yake hivyo basi mpaka wakati huu elimu anayokuwa nayo ni ya lugha ya Peponi na ile anayokuwa ameanza kupata Chuo Kikuu kabla ya ujauzito.Elimu ya ziada aliyonayo ni ile ya fundisho kutoka kwa Malcom X na Lawino wa Okot p'Bitek katika *Song of Lawino* and *Song of Ocol* ukurasa wa 40 ambayo imemfungua fikra,mafundisho mengine ni kutoka vitabu anavyovisoma mwenyewe kama cha Deborah Tannen,*The Argument Culture* na riwaya ya Alaa Al Aswany,*The Yacoubian Building* na cha Mreno Jose' Saramago.

### 2.2.13 Mfanyibiashara

Afida ni fundi wa kuchonga vinyago na kufuma vitambaa vya mapambo kutoka kwao Motoni na anautumia kupata nyongeza ya pesa za kumhudumia Mkombozi kwa kuunza vifaa hivi, (ukurasa 185) .Uhusiano wake na Mkombozi unaendelea kuwa wa afya kwani anayakidhi mahitaji ya Mkombozi yote kwa kupata nyongeza hizi za pesa.

### 2.2.14 Afida anaithamini na kuitumia lugha

King'ei (2010) anaeleza kuwa,lugha ni zao la jamii na ni kipengele muhimu sana cha utamaduni wa jamii husika na hutumiwa na jamii kuhifadhi amali na utamaduni wake hasa kama chombo maalumu cha kuwezesha wanajamii kuwasiliana vilevile ni njia inayotumiwa na wanajamii ili kueleza na kusambaza utamaduni wake.Mwanadamu hawezi kufikiri kamwe bila kutumia lugha. Hii inamaana kuwa kwa lugha ni muhimu sana katika maisha ya binadamu kwani mawazo na fikra za mwanadamu vinawakilishwa na lugha.Hivyo tunawaona Shuhuda na Afida wakidhamini lugha yao asilia kwani ndiyo wanayoitumia katika basi kuwasilisha mawazo yao.

> “Mara kadha wa-Peponi waliokuwemo basini,waligeuza shingo kututazama jinsi tunavyoropokwa na kuistaajabia lugha tunayozungumza.Lugha yenye kelele namna hiyo.Walishangaa ingawa hata wao wakikutana katika vuguvugu la hamasa namna hivi,huzungumza lugha yao kwa kelele zinazokera.” (uk 77)

### 2.2.15 Amejitenga na mamake

Afida amejitenga kiroho na mamake kama babake anavyosema Afida anajificha katika dunia yake,hakumbuki fadhila/ hisani na kuwa damu moja na mamake Bi.Mwamda, (uk. 120)

### 2.2.16 Mpishi bora

Afida anakuwa mke na mama mtoshelezi kwa mume wake na mtoto wao.Ni hodari wa kupika vyakula vya kienyeji kama pilau,biriani,mseto,wali wa kunde,wali wa asumini,mikate ya maji,kitumbua,n.k. (Uk. 166).

## 2.17 Hitimisho

Katika sura hii tulizungumzia uhalisia uliyopo katika familia za kiafrika kwa kuangazia hali iliyopo ya Afida na kutathmini kuwa imezuka kwa ajili ya mahusiano mapya yanayozuka katika maisha yake Peponi na kuielewa hali hii asilia kutufungua macho kuona kuwa imeathirika na usasa uliopo. Hali hii ni dhairi katika familia za kiafrika kwani uhalisia huu ndio ulipo katika jamii ya leo.Muhtasari wa riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* umewasilisha uchangamano wa maisha ya Afida ambao unaleta misukosuko katika mahusiano yake na familia.

## SURA YA TATU

## USASA WA FAMILIA ZA AFRIKA

### 3.0 Utangulizi

Kupitia masomo, maingiliano ya tamaduni,hali, ujuzi na maarifa ya binadamu kuongezeka, binadamu amevumbua vitu vya kisasa ambavyo vinachipuka kutokana na fikra hizi mpya, mitazamo mipya ya mambo na hali mpya ya maisha kama uvaaji, starehe, ajira matibabu na hata usalama,na hii ndiyo sababu tunakumbaliana na Suakei (2013:51) anapoeleza usasa kama

> "Kuendelea kwa binadamu kulingana na jinsi ulimwengu ulivyo kunatengemea anavyowaza, anavyoshughulikia ulimwengu na bidii aliyo nayo ya kwenda sambamba na ulimwengu unavyosonga mbele."

Watu sasa wamo katika ulimwengu unaoharakisha mabadiliko ya kitamaduni kiwakati,wakisukumwa na kupanuka kwa biashara kitaifa,vyombo vya habari,utalii,masomo na kuongezeka kwa idadi ya watu miongoni mwa mambo mengine.Utamaduni wa kigeni na maendeleo ya kiteknolojia yanaweza kusababisha mabadiliko katika jamii kwa kubadilisha mikikimikiki ya kijamii kwa kukuza ruwaza mpya za kiutamaduni kwa kuwezesha tukio zalishi.Hii mihamisho ya kijamii huweza kuandamana na mihamisho ya kiitikadi na aina nyingine za mabadiliko ya kitamaduni.Kwanza, kuna kubadilishana mawazo kwa kurejelea elementi za utamaduni mmoja na ambazo husababisha kuwepo kwa uvumbuzi mpya wa mambo.Pili, kuna ukopaji wa moja kwa moja yaani kusambazwa kwa arki za utamaduni wa jamii moja kwa nyingine.Huku ni kuiga tamaduni kwa kubadilisha tabia fulani za utamaduni mwingine. Haya yote yanachochewa na watu wa tamaduni mbalimbali wanapojikuta wakiingiliana pamoja viwandani,maofisini,safarini,vyuoni na kwingineko.Hii ni katika hali ya binadamu kutaka kujua zaidi kwani mawazo yake yanapanuka kutokana na kukua kwa akili na hivyo kutaka kujua kuhusu watu wa tamaduni nyingine ili kuhusiana vyema zaidi .

Na hiyo ni kwa sababu kila uchao mambo mapya huibuka na kumwathiri binadamu kwa njia nyingi.Kwanza, kuna kuiga utamaduni wa kigeni kwa namna mbalimbali.Katika familia ya *Mhanga Nafsi Yangu* usasa unaelezwa kwa jinsi babake Afida aliyekuwa kielelezo kwa Afida

alipokuwa hai na hata mautini alihusudiwa na Afida kwa upole wake, uchangamfu wake,elimu yake ya mchanganyiko wa maisha na vitabu. Baba Afida aligundua usasa upo na una athari ndipo alipomtayarisha mwanaye ili aweze kukabiliana nao. Afida anasema,

> "Tokea utotoni wangu, baba alijaribu kuniosha na kunisuuza ili nitakate. Alitaka niwe kiumbe safi chenye kufikiri na kuamua vizuri kabisa lile linalofaa na lile lisilofaa."( Uk. 111).

Ni dhahiri kuwa mitagusano hii imezipelekea familia za Afrika kuwa na usasa na hii ndivyo Said A. Mohamed anaeleza uhalisi huu katika riwaya hii.

## 3.1 Usasa

### 3.1.1 Mahusiano ya ngono nje ya ndoa

Ngono kabla ya ndoa inatazamwa kama jambo la kawaida,na hakuna kuhisi hatia yeyote ya kuwa na uhusiano huu.Afida anajiingiza katika ngono akiwa bado chuoni,hali hii inatokana na ushawishi wa marika na hali mpya ya Peponi.Kushirikiana katika ngono kabla ya ndoa kumejitokeza kwani . Afida anajisabilia kwa Neshboch na kuhusiana naye kingono kabla ndoa yao haijarasimika (uk. 146), Afida anafikiria ngono kabla ya ndoa ndiyo njia pekee ya kujenga na kudumisha uhusiano wake na Neshboch na kwa kuwa Neshboch kuwa 'lifetist' na kuiona ngono nje ya ndoa kama inastarehesha yeye na Afida wanageuza lengo la msingi la ngono la kukifanya kitendo halali na kuendeleza kizazi cha hiari baina ya watu wenye uhusiano halali na unaoeleweka.

### 3.1.2 Hali ya maisha mapya ugenini

Majira ya baridi ni hali mpya anayokumbana nayo Afida huko Peponi kwani alipo sasa hawezi kulala kabisa,hawezi kulala mchana wala usiku kwa hiyo, baridi kali inayomkandamiza kitandani pake ina ufukuza usingizi kwa kuwa analala kwenye kijichumba chenye baridi ya kifo huku shangazi yake Bi.Marneti na mumewe Bwana Bawa, wakiishi kwenye chumba kikubwa kilichojaa uvuguvugu na raha,(ukurasa 26). Pia Afida anakatazwa kukoga kila siku au kukoga asubuhi na jioni kama alivyozoea kukoga kwao Motoni na Bi.Marneti kwani anamweleza Afida kuwa kwanza, Peponi hapana joto kama Motoni na pili Bi.Marneti anaiona kama Afida anataka kuwa mweupe kama Wapeponi. Zaidi ni kwamba, maji ni ghali Peponi kwani kila tone linalodondoka lina thamani kubwa ya pesa.Vilevile Motoni watu wanathamini urafiki hasa watu wa Peponi tofauti na ilivyo Peponi ambapo Mpeponi huwa rafiki yako pale anapokuwa na haja,akishapata anachokitaka, si rafiki yako tena, (uk 90).

### 3.1.3. Asasi ya ndoa na falsafa yake

Ndoa na uamuzi wake unatokana na mbolea katika mazingira ya kifamilia hasa uono wa wanafamilia ni kulingana na uamuzi kulingana na daraja hii muhimu maishani,ndipo Afida anachukua mawazo ya Bi.Marneti kuwa yenye umuhimu katika kufanya uamuzi wake kwa kuwa yeye ni familia na huo ndio umuhimu wa kwanza na pili ni kinachoziba pengo la utashi nafsini mwa mtu na kwa kumrejelea Afida ni utashi wa mali na uraia wa Peponi na utashi huu mpya umechangiwa na uchangamano wa maisha ya usasa maishani mwa Afida.Na hivyo Bi.Marneti anapompigia Neshbosh ngoma ili awe na uhusiano na Afida,Afida anakubali ilhali Neshboch ana miaka sitini na mbili anasahau hali ya maingiliano katika asili yake Motoni kwani Neshbosh ni mzee anayeweza kuwa baba ya Afida ambaye ni kigori na anasukumwa na mawazo ya shangaziwe na utashi wake mpya kuliko kuzingatia mikabala muhimu katika uhusiano hasa kutokana na tabia za Neshbochkwani mara ya kwanza anamwonyesha ujeri na kumdhalilisha pale mezani kwa Bw.Bawa kwa kupenyeza miguu yake chini ya kiti na kuanza kunyemelea eneo la mwili wa Afida hatua kwa hatua,jambo linalomfanya Afida kuandoka mezani kwa chuki huku akisusia chakula lakini shangazi yake Bi. Marneti hajishughulishi na kumuuliza Afida chochote,( uk 140).Na baadaye anamwambia Afida kukubali kuolewa na mzee Neshbosh kwani ana mali nyingi ya kumweka Peponi, na hata atampa uraia wa Peponi.Motoni mchumba angeruhusiwa hata kumkubatia mpeziwe mbele ya mama mkwe au jamaa zake. Anauumbua uhusiano wa Afida na Yakrobich ambaye walikuwa na maingiliano ya afya na yaliyo mrithisha Afida kama alivyotueleza.Bi.Marneti anamweka Yakrobich chini ya Neshboch kwa kumweleza Afida kuwa,

> “Yakrobich si marafiki, ni upepo wa kupita tu, wanaotaka kumzoazoa mwanamke na kumtupa chini na kumkandamiza…hawana lengo lao wenyewe”.

Huu ni uvumi wa kumpujua Yakrobich kwani mara kwa mara Yakrobich alimpeleka Afida kwenye burudani kama sinema, *disco*, *parties* na mechi za *golf*.

### 3.1.4 Mikataba ya ndoa

Neshboch na Afida wanaamua kuishi pamoja kabla ya ndoa, na wanapoamua kuingia katika mkataba wa ndoa, hakuna sherehe kubwa inayofanywa. Inafunganishwa mchana kama ilivyo kawaida ya usasa, wanaenda kwa katibu ili kupata kibali tu cha ndoa badala ya kanisani au msikitini na suala la mahari halizingatiwi kinyume na utamaduni asilia wa Afida Motoni

.Muhimu katika mkataba huu si mapenzi bali ni kile ambacho kila mwanandoa anachotarajia kupata katika kufunga pingu hizo za maisha.

Mikataba ya ndoa huhitimisha kifungo cha ndoa ambayo husisitiza kukubali kuwa pamoja katika dhiki na furaha. Mtindo huu mpya wa mkataba wa ndoa unaotokana na jamii ya sasa ambayo imeweka mipaka katika mahusiano ndani ya ndoa katika sheria, kwa maana kuwa ndoa inaweza kuvunjwa kulingana na sheria. Mkataba wa ndoa unahusu kudhibiti masuala yote ya mali na watoto ili kujaribu haleta haki baada ya kusambaratika kwa uhusiano.Hivyo Afida anaingia katika mkataba wa ndoa na Neshboch hii ni kwa kuwa baada ya ndoa yao kufikia kikomo hakuna kushiriki mgawanyo wa mali kwa hivyo hakuwa na umiliki wa pamoja wa mali yao katika mkataba wao wa ndoa na haya ni kwa mujibu wa maamuzi ya sheria. Ni muhimu kutaja kuwa Afida hakuwa amefikiria juu ya hitimisho la mkataba wao wa ndoa na ndio maana anapoteza kila kitu.

### 3.1.5 Ndoa za mchanganyiko

Ndoa ya mchanganyiko ni kawaida Peponi kwa sababu Bi.Marneti na Bw.Bawa wanakuwa katika ndoa hii hata kabla ya Afida kufika Peponi lakini jambo hili halipo Motoni.Ndoa ya Afida na Neshboch ni ya mchanganyiko kwa sababu Neshboch ni Mpeponi mweupe na Afida ni Mmotoni mweusi.Ithibati tosha kuwa hii ni ndoa ya mchanganyiko ni wasifu wa Dinda (mtoto wao) ulikuwa wa mchanganyiko,amepata rangi ya maziwa kwa babake,nywele nyeusi ndefu kama za mawimbi za mchanganyiko wa mama na babake, (uk. 164).

### 3.1.6 Magonjwa

Kuna magonjwa ya kisasa yanayomkumba Afida.Kwanza, anapatwa na kitetemeshi cha mwili na mafua makali inabidi apelekwe hospitalini na shangazi yake Bi.Marneti.Mafua yanatokana na majira ya baridi ambayo ni  mapya kwa Afida.Daktari zahanatini anasema watu wengine hufa kwa mafua Peponi, (uk. 37).Pia Afida anagunduliwa kuwa na saratani ya fuko la uzazi hospitalini baada ya kufanyiwa uchunguzi na daktari kutokana na kuhisi maumivu makali tumboni anapokuwa akichonga kinyago ili kuuza apate pesa za nyongeza kumhudumia Mkombozi.Anafanyiwa operesheni na anapona.

### 3.1.7 Mihadarati

Kwanza kuna ulevi ambao ni ulemavu tegemevu wa kudhuru wa pombe na pia ni usasa ambao ni swala nyeti katika familia licha ya kuwa ugonjwa unaoweza kutibika.Dalili zake ni kunywa pombe kupindukia bila udhibiti licha ya ufahamu wa athari zake.Utumiaji huu wa pombe 'vibaya' hunamiliwa na kutegemea pombe kupita kiasi licha ya kufahamu athari nyingi zake. Afida ni mraibu wa pombe,anakunywa pombe kupindukia bila udhibiti pombe licha ya kusema hatafanya hivyo.Utegemezi huu wa pombe umetokana na kubadilika kwa mazingira yake,mfadhaiko wa ubongo na kupokonywa mwanawe Dinda na Neshboch. Pili kuna uvutaji sigara na vijana wengi wamekuwa wakijiingiza katika uvutaji huu kwa kufuata mkumbo unaotokana na mkazo mkubwa wa mtu binafsi. Shuhuda huvuta Sigara kila mara kutokana na msukumo wa usasa wa Peponi.Hali hii inajitokeza Afida akiwa basini anapotueleza sigareti haimtoki Shuhuda vidoleni kwani akimaliza hii,huwasha hii, (uk. 71).Vilevile ndani ya mkahawa wa Zaman Afida anapuuzilia mbali utashi wake wa kujaribu kumkataza kuvuta sigara yake kwa kuwa anasema kumwambia azime sigara yake ni kama kumwambia asitishe moyo wake, (uk 85).

### 3.1.8 Mavazi na mapambo

Familia mpya sasa inahubambiza usisi kabla ya umimi kwa kuambiwa wazi kwamba kama tunakata kuwa na tamaduni za kigeni lazima kupokea na kuukubali tabia na mwenendo na desturi zao.Wanakuongoza kwenda uchi au kuvaa nguo, kuiga mitindo fulani kwa mfano kwenye Taasisi za elimu na vyombo vya habari, na mashindano ya feshini kama *Miss World* na kwa Shuhuda ambaye asilia, yake ni Motoni kuvaa nguo za kubana na za kisasa anazojua kuzichagua na jinsi ya kuzivaa ili aonekane mwanamke wa kileo. Nguo hizi ni kifulana chenye kuteremka chini kidogo na kuacha kwa makusudi upasu, (uk. 72).Ameanza kuvaa mtindi wa kisasa kwani anatueleza vile baridi ilivyomzidi hadi mikono yake aliyoivisha glovu aliizama mifukoni mwa suruali au jaketi kabla haijatolewa nje kuwiana na miguu yake, (uk. 89). Pia kuna usasa wa kuongozwa na teknolojia ya kutia malengelenge ya mchanga ili kukuza matiti,kugeuza macho kijapani katika ukurasa wa 79.

Kulingana na utamaduni wa Kipeponi mwanamke lazima aonyeshe mwili wake kama anataka kufanikiwa. Kama alivyofikiri shuhuda, (uk 73). Mfano wa nguo hizi ni kifulana chenye

kuteremka chini kidogo na kuacha kwa makusudi upasu, *"minisketi" 'leggings'* na *gloves* za nusu vidole na ndio maana Shuhuda anaathirika na usasa huu kwani anaambukizwa virusi vya ukimwi.

### 3.1.9 Vifaa vya nyumbani

Teknolojia ya kisasa imerahisisha maisha kwa kiasi kikubwa.Wahandisi wetu wametumia weledi na maarifa ya kisayansi kuunda vifaa vipya ambavyo vimerahisisha kutenda kazi na hiyo ndiyo sababu ndani ya nyumba ya Afida na Neshboch mna vyombo vya matumizi ya nyumbani kama vile friji,jiko la umeme,*microwave*,mashine ya kufulia,mashine ya kuoshea vyombo na vifaa vingine kadha, (uk 166). Hivi vyote vinavyomwondoshea binadamu udhia wa kujituma kwa kurahisisha aushi ya binadamu katika kutenda kazi. Vyombo vya mapambo picha na sanaa nyingine vya kutuliza roho zilikuwemo pia

### 3.1.10 Usafiri

Usafiri wa kisasa unajitokeza wakati Afida anapata 'bahati' ya kwenda Peponi.Anatumia usafiri wa kisasa ambao ni ndege *ya Air Uropa*, (uk. 1).Njia hii imefanya maisha kuwa mepesi na ya furaha,kwani Afida anasafiri kwa wepesi Peponi yaani kwa muda mfupi ikiliganishwa na kutembea kwa miguu au kwa kutumia wanyama.

### 3.1.11 Malezi

Kuna watoto ambao wazazi wao hawawataki na ndipo huwekwa katika nyumba ya malezi ya watoto wasiotakiwa na wazazi wao kwa malezi na hapa huwekwa watoto wasiowezwa kutuzwa na wazazi wao kwa sababu moja au nyingine, kwani hapa ndipo Mkombozi anapowekwa kwa muda mpaka Afida atoke hospitali baada ya kufanyiwa oparesheni, (uk. 185). Wazazi ndio wanaojenga msingi wa tabia ya mtoto lakini Afida ameasi ulezi aliyoupewa na babake hivyo amebadilika kwani anamjibu babake kwa kumwambia wako katika dunia tofauti naye amejaa ukale.

Katika asili ya tamaduni za Afrika watoto wa kike hawakupewa uhuru. Lakini kutokana na babake Afida kuathirika na ujio wa dini ya kiislamu, hasa katika kusoma vitabu vya dini hii alimpa Afida uhuru. Afida anasema, "Nilimhusudu kwa upole wake,uchangamfu wake,elimu yake ya mchanganyiko wa maisha na vitabu,hasa vilivyoandikwa kwa hati za Kiarabu,"(uk 11).Vitabu hivi vinampa babake Afida ana mtazamo mpya na anafanya uamuzi wake wa kumlea

bintiye tofauti na kaida za utamaduni asilia na wala hambagui kwa kuwa mtoto wa kike na ndivyo anatueleza;

> “Natumai unakumbuka uhuru niliokupa siku zote maishani mwangu.” “Nakumbuka na nawashukuru baba.” “Si mababa wengi wanatoa uhuru kwa watoto wao namna hiyo, hasa watoto wao wa kike”.

Na hivyo uhusiano kati yao unaathirika,babake anakuwa ruwaza kwake akiwa hai na mautini kwani alifuata yote aliyomwambia na kumheshimu.

### 3.1.12 Hali mpya ya maisha Motoni

Mabadiliko yametokea katika usiku mtulivu wa Motoni na kuwa ni wakati wa raha kwa wenye pesa zao, huwa kwenye vilabu vya pombe, *Casino*, hoteli kubwa wakifakamia vyakula, kunywa na kulala na wapenzi wao, (uk. 104).

### 3.1.13 Muziki

Katika burudani mbalimbali kuna muziki. Muziki ni muhimu sana katika maisha ya binadamu kwani umejichopeka katika shughuli za kila siku. Miziki yenye kuiga usasa ndani yake mfano.

> “Ngoma iliyoitwa benibati (au koboka) iliyochezwa na watu waliovalia suruali vipande, mashati meupe ya mikono mifupi, mabuki miguuni na *stockings* mpaka Magotini, (uk. 130).

Hapa wameiga malemba ya jamii/utamaduni wa ugenini. Ikitofautishwa na muziki ulioiga tu maneno ndani ya wimbo lakini mambo mengine yote ni utamaduni asilia wa Motoni. Mfano:

> “…baadhi ya siku ilipigwa ngoma ya bomu la wanaume lililochezwa katika mzunguko wa duara ya bakora au kigongo begani. Katika bomu la wanawake wapambe walicheza wakiwa wamevaa mavazi ya kuchekesha, (uk. 129).

Kuna wimbo maarufu walioupenda katika bomu ambao uliwakirihisha wazazi Kama Afida anavyotueleza ni kuwa wamotoni ndiyo kama jamii zingine zilivyoiga lakini waliiga kwa kuujali utamaduni wao nahali za maisha yao zilivyo katika wakati fulani.Kuna nyimbo za kizazi kipya kama wa Marvin Gay, ‘*Whats Going on’*? Uliochezwa na Afida na Yakrobich katika ukumbi wa Taasisi ya Lugha Peponi, (uk 131).

### 3.1.14 Usakaji wa elimu ya kisasa

Inamlazimu Afida kusoma masomo ya miezi tisa ya lugha ya Peponi anapofika tu Peponi kwani wanafunzi wote wageni lazima kuisoma lugha hii kabla ya kuingia katika masomo mengine yeyote.Lugha ya Peponi inachukuliwa kuwa ngumu kwa 'Wageni' kutokana na uono wa Wapeponi.Idhibati tosha ni kuwa Afida ndiye anayekuwa mwanafunzi wa kwanza wa Motoni kufaulu vizuri Kipeponi tokea miaka kumi na mitano iliyopita.Uk 96. Anasoma vitabu vingi kama riwaya za Alaa Al Aswany, *The Yocoubian Building* na ya Jose Saramango. *Blindness*.Hili Afida aweze kupima jinsi waandishi wanavyoitazama dunia.Elimu mpya ya vitabu inamfanya Afida kupata falsafa mpya ya maisha kwa sababu analiganisha mambo kwa falsafa za kisasa kama anavyosema kuhusu vitu anazungumzia DBC Pierre anavyosema, *Look at it,my friend:all has ever been called love of life,is a love of things that won't happen*, (uk 95).

### 3.1.15 Amali za jamii kulingana na usasa

Kuna sherehe za siku za kuzaliwa kama mmojawapo wa amali zinazofanywa na Wapeponi. Tunamwona Neshboch akifanya sherehe kila uchao za siku yake ya kuzaliwa ili kumvuta Afida kwa lengo la kuanza uhusiano naye. Sherehe hizi zinafua dafu kwa kiasi kwani Afida anatabua kuwepo kwake lakini hakubali uhusiano naye katika sherehe.Baada ya kuzungumziwa na Bi.Marneti ndipo aakubali.

### 3.1.16 Tabia zisizoeleweka

Tabia za mhusika mkuu zinaashiria hali isiyo ya kawaida.Afida ana uwezo wa kuzungumza na sauti zake mbili kwenye fikra zake,na zaidi kufanya mjadala nazo.Kuweza kuingia akilini na kufanya mijadala nyeti na sauti mbili tofauti zenye mitazamo na falsafa tofauti kuhusu maisha yake binafsi inaashiria ni mandhari yasiyo ya kawaida.Hali hii inatudhihirishia kuwa Afida yuko katika njia panda kwani hajui kama ataiga usasa au kudhibiti utamaduni.

### 3.1.17 Mawasiliano ya kisasa

Kupitia kwa sayansi na teknolojia mpya,kuna mawasiliano baridi kupitia kwa mitambo ya tarakilishi na rununu hivyo watu hutumiana ujumbe wa kusomwa kwa kubofyabofya vibonyezo kwenye simu tamba au kwa barua ambazo ni matokeo ya teknolojia mpya kama nukulishi na mdahilishi ikitofautishwa na mawasiliano joto ambayo. Afida anatumia kuwasiliana na familia yao Motoni kwa kuzungumza wakikaribiana kwa sauti wakitumia lugha ya kuelewana.

Ikumbukwe baadhi ya vyombo vya mawasiliano vinavyoendeleza haya ni redio, runinga, rununu, mtandao.wavuti, na vinginevyo. Kwa mfano, Afida anawasiliana na Shabani kwa kutumia

rununu inayomwezesha kufahamu kuwa Shabani yuko hospitali katika chumba cha watu mahututi.

### 3.1.18 Utandarithi

Hii ni jinsi maisha inayoendelea kuutwala ulimwengu wote katika karne hii ya 21.Utandarithi ni utamaduni uliotanda au kuenea ulimwenguni kote.Mtu mtandarithi hivyo basi ni mtu aliyebobea kikamilifu katika utamaduni huu mpya kwa jinsi moja au nyingine.Mtandarithi hujihusisha sana katika kutandaridhisha aina moja au nyingine ya amara muhimu za kitandaridhi.Hizo ni kama vile biashara za kimataifa,lugha za kimataifa aina za mavazi zilizotokea kupendwa ulimwenguni kote,muziki wa siku hizi,kama vile pop,reggae,raga,rap,ambao asili yake ya hivi majuzi ni Marekani. Afida ni mtandarithi kwani anapenda muziki wa aina hii kwani anapousikia mdundo wa muziki wa fanki (funk) akiwa chumbani mwake anasoma muziki huo ulitekenya nafsi yake .Hisia zilizotokota na hatimaye kuhaha na kuvundumka nani ya damu yake.anasema tone moja tu la muziki huu lingeweza kumnyanyua na kumfanya aogelee milele ndani ya bwawa hilo la muziki akiwa amepagawa.Uk. 161.Alipenda muziki wa Jazz,Soul,Blues,Twist na Rock n'roll pia.Uk 131. Kwa upande mwingine Afida anaitandarithisha lugha ya Kipeponi kwani anakuwa mwanafunzi wa kwanza wa Motoni kufaulu Kipeponi tokea miaka kumi na mitano iliyopita na hata anatoa hotuba ya shukrani kwa Kipeponi. Anaitumia katika mahusiano yake ya kila siku na familia yake Peponi,yaani kuwasiliana na Neshboch,Dinda,She-shaiza na Bendelheib.

## 3.2 Hitimisho

Hali hii ya usasa na tulizozitaja hapo juu ndizo zinazaothiri mahusiano ya familia na ndizo zinazoleta mageuzi katika mahusiano haya huku zikiathiri familia za Afrika. Hii ni kwa sababu watu sasa wamo katika ulimwengu unaoharakisha mabadiliko ya kitamaduni kiwakati,wakisukumwa na kupanuka kwa biashara kitaifa,vyombo vya habari,utalii,masomo na kuongezeka kwa idadi ya watu miongoni mwa mambo mengine. Pamoja na hali kuwa utamaduni wa kigeni na maendeleo ya kiteknolojia yanaweza kusababisha mabadiliko katika jamii kwa kubadilisha mikikimikiki ya kijamii kwa kukuza ruwaza mpya za kiutamaduni kwa kuwezesha tukio zalishi.

## SURA YA NNE.

## ATHARI ZA USASA KWA FAMILIA ZA KIAFRIKA NA CHANGAMOTO ZINAZOIBULIWA

### 4.1 Utangulizi

Sehemu hii inaangazia athari za usasa zinavyoathiri mahusiano katika familia za kiafrika na changamoto zinazoibuliwa na athari hizi.Athari hizi zote tumeziangazia kwa kukita matini rajelewa.

### 4.2 Kubadilika kwa ukubwa na muundo wa familia

Familia ya kiafrika iliyoundwa na baba,mama,watoto pamoja na ndugu wa baba na mama akina babu na bibi imevunjika na kuwa familia ndogo ambayo ina wazazi na watoto wao na baadhi ya jamaa tu,si ukoo mzima.Mahusiano ya ukoo yametoweka na shughuli wanazotekeleza.Kwa mfano,siku zile Afida alipokwenda shule bila ya kupata kisabeho kwa sababu wazazi wake hawakuwa na senti nyekundu,alikuwa akimpitia shangazi yake nyumbani kwake.Afida siku zote hakuambulia patupu kwa bibi huyo-kama si vya mwiku ,basi mkate wa boflo wa leo asubuhi na chai ya mkandaa. Alipokuwa hana chakula chochote cha kumpa na ilipotokezea kwamba ana visenti vichache, basi Bi.Sinangoa alijifundua kibindoni,akatoa walau kigwaru cha senti hamsini na Afida aliweza kununua boflo na mboga na mboga ya kisambu na mbatata za rojo shuleni.uk. wa 8.Hapa inaonyesha ukoo ulikuwa na mahusiano ya karibu,yaliyokuwa ya kijali maslahi ya kila mmoja kuhakikisha ana mahitaji ya kimsingi,watoto walikuwa pamoja,walifanya kazi pamoja na walifaidika pamoja.Kama baba Afida kila Alhamisi kuamkia Ijumaa,baada ya sala ya Magharibi ,alitukusanya sisi watoto wa nyumbani na watoto wa majirani na mitaani kutusikikiliza jinsi tulivyoendelea kuhifadhi sura za kitabu kitakatifu na jinsi tunavyopanuka kimaadili ya dunia katika mwelekeo wa ahera.Mapema sana udogoni mwetu,alitufundisha ile aliyoita abjadi au alfabeti, (uk. 111).Aliakikisha walikua pamoja kwa kuwafunza kwa pamoja na hivyo wote kufaidika na elimu yake. Mambo yamebadilika kwani Afida anaposafiri Peponi na kuathirika na utamaduni wa Peponi, hasa anapotawazwa umalkia na Neshboch, pesa na neema zilimzunguka kila kipembe na kutumiwa kwa na furja hivyo kuweza kupata kila kiti alichohitaji bila kutegemea ukoo, hakumbuki ahadi za kusaidia ukoo wake alizopeana na hivyo kuvunja

uhusiano wa familia hii yake kubwa kilicho muhimu kwake ni kutimiza majukumu yake kwa mumewe Neshboch na mwanawe tu.

Ukoo ndio uliotafiti kwa kina juu ya mwelekeo wa mposaji na anayeposwa uk wa 150.Hili kuhakikisha mposaji ni kukubali watakaoana .Harusi ilihusisha ukoo wote hata zaidi marafiki, majirani, wa karibu, wa mbali na wapiti njia.Afida katika hali ya kuanza uhusiano na Neshboch hakuna utafiti wa kina juu ya mwelekeo wa Neshboch uliofanywa na familia ndoa ilikuwa ni kwa sababu ya tamaa mpya ya Afida inayotokana na tamaa ya mali nyingi na uraia wa Peponi.

### 4.3 Kuibuka Familia iliyoongozwa na mwanamke

Wanaume ndio siku zote walioziongoza familia zao kwa kuchumia familia zao kama babake Afida alivyowachumia kutokana na yeye kuwa mganga maarufu, (uk. 12). Lakini tunaona kutokana na kuvunjika kwa ndoa ya Afida na Neshboch imemlazimu kwani gharama za kumchukua mtoto kwa hali na mali anazibeba yeye mwenyewe hata alitumia ufundi wake wa kuchonga vinyago na kufuma vitambaa vya mapambo na kuviuza ili kumhudumia mwanawe Mkombozi, (uk. 185).

### 4.4 Utengano

Maingiliano ya Afida na mamake yameathirika na kama anavyofafanuliwa na babake katika ukurasa wa 120.Yeye na mamake wamejitenga kimwili na kiroho kwani hakuna mawasiliano yoyote kati yao. Kila mtu anameshika lake bila kujishughulisha na maisha ya mwezake (Afida na mamake),

> "hakuna anayekumbuka fadhila au hisani au ya damu moja iliyouma kuliko kitu chochote."

Hapa Afida ameathirika na usasa ambao kila mmoja anajishughulisha na maisha yake mwenyewe hasa mambo ambayo yanaleta manufaa kwake yeye mwenyewe.Hii ni kwa maana Afida anajaribu kueleza dhana ya uchangamano wa usasa kama kutaka makuu, kupigania viwango vya maisha yaani (living standards) isishuke chini kwa hali yoyote ile, milka ya vitu, mamlaka, mavazi,(uk. 120).Mambo haya yote ameyaelewa amekumbana nayo na hata yamemwathiri na hasa hapa yameathiri uhusiano wake na mamake na pia yanamfanya asijue nini maana ya furaha kama tunavyobainishiwa na babake mzazi.

Maingiliano ya Afida na Bi. Marneti yanaathirika kwa pesa za matumizi anazompa hazimtoshi, zinafika kifundoni tu kwenye mahitaji ya Afida pekee hakuweza kulipa kitu chochote zaidi kwa

sababu hakuwa na senti nyekundu ya kumlipia mtu yeyote, (uk. 85). Ndio maana Afida alimruhusu Saparata kumlipia chakula na vinywaji hasa walipokuwa mkahawa wa Zaman.

### 4.5 Kuvunjika kwa ndoa

Motoni wanawake hawana hadhi kama Bi.Mwamda anavyomwelezea Afida kuwa mwanamke kama yeye hana sauti na hata Afida mwenyewe alifahamu kuwa mwanamke ana uhuru huo, (uk 14).Ndoa nyingi zimefikia kikomo kwa sababu Peponi sheria imeongezea hadhi ya mwanamke katika familia,swala ambalo limechangia kuhitimisha ndoa kwa kisingizio kuwa ndoa hairidhishi kama ilivyo ndoa ya Afida na Neshboch inapofikia kikomo kwa maagizo ya mahakama iliyomkandamiza na kumwangusha chini Afida na kumpa Neshboch haki ya kukilea kitoto chake Dinda, (uk. 172).Kikomo cha ndoa kinaathiri mwanamke na inamtia waa mwanamke kwa kupunguza hadhi yake katika jamii na kunyweza mfumo wake wa kujihimili na hivyo basi talaka kwa Afida zinamfanya kupoteza imani na uhai wake katika ukurasa 173 na hata kupoteza mwili wake kwa jinsi anavyoshindwa kuzuia tabia ya kunywa pombe kwa wingi na aliposhiriki ulevi,ulevi ulimkaushia pes ambazo hana na kuingia katika mtengo wa kukaribisha ulevi na wanaume kwa mtindo wa nipe nikupe.Akawa hatoki tena kwenye baa kuwafuata wafadhili wake ambao nao walitaka kufadhiliwa, (uk 176-177).

### 4.6 Ushiriki wa wanawake kiuchumi

Mfumo wa kiuchumi umewezesha wanawake kuwa huru kutokana na kazi za kinyumbani na kuingia katika kazi sokoni.Soko limebuni namna mpya za kupunguza kazi,na hivyo kuwawezesha wanawake wanaenda maeneo ya kazi na hata kuzifanya kazi,Afida anapotumia ufundi wake wa kuchonga vinyago na kufuma vitambaa vya mapambo na kuviuza hivyo anapata fursa ya kubadilisha uzoefu na kipaumbele katika maisha yake,huku akipata changamoto ya kusimama kidete kukabiliana na changamoto pamoja magumu yanayomsibu.Hivi Afida anajaribu kukabiliana na umaskini kwani anafaidika na anachozalisha.Hii ni changamoto kwani anajaribu kutekeleza haya akimlea mwanawe kwa pamoja hata anapogunduliwa na saratani ya fuko la uzazi hawezi kukimu mahitaji ya mwanawe akiwa hospitali ndio sababu inambidi mwanawe Mkombozi awekwe katika nyumba ya malezi ya watoto wasiotakiwa na wazazi wao kwa muda mpaka Afida atoke hospitali baada ya kufanyiwa operesheni, (uk. 185).

### 4.7 Uhasama kati ya jinsia mbili

Katika uhalisia wa Peponi kulikuwa na mgawanyo wa kazi na matakwa kwa kila jinsia, wanawake walipika,ulezi wa watoto na shughuli nyinginezo za nyumbani,kwa mfano Afida alimlea Kisura baada ya kifo cha Sada aliyefariki, (uk. 11). Bi. Sinangoa anamwinjikia Afida chai mekoni ili apate kisabeho baada ya wazazi wake hawakuwa na senti nyekundu.Wanawake hawazungumzi mbele ya umati wala kufanya maamuzi makali ya kifamilia Afida anaonyesha haya anaposema,

> "Udogoni mwangu, mara nyingi niliambiwa na wazazi wangu nijizuie kujibu anaposema mtu…lazima niziweke flkra zangu ndani mwa nafsi yangu.Niziweke zisitoke nje kuja kumtusi hata anayebananga," (uk. 11).

Familia mtazama msichana wao kwa karibu na kama kuna shida wanaingilia na kuitatua.Wanaume nao walitoa ulizi, walifanya maamuzi kuhusu maswala muhimu ya familia,na kukimu mahitaji yote ya familia kama alivyofanya marehemu babake Afida kabla ya kifo chake.

### 4.8 Uhamiaji wa kimataifa

Afida anahama kutoka kwao kwenda Peponi akisukumwa na haja ya kukimu ukoo wao mkubwa ambao anaupa ahadi kabla ya kuondoka.Uhamaji huu unatokana na usasa wa wanawake kuwa chombo cha uchumi .Hii ni kwa sababu katika familia za kiafrika lazima uhamaji unasababisha utengano na familia yao na uhalisia katika familia hivyo hali mpya katika usasa huu inaonyesha kuwa Afida hana kazi,hana chochote anachokichuma mwenyewe.Anategemea pesa anazopata ni zile za matumizi anazopewa na Bi.Marneti na hazitoshi hata mahitaji yake,(uk. 85). Hali hii inamsukuma kuwajibu wachache tu tena kwa nadra wanaomwandikia barua mfululizo tokea ahamie Peponi kumjulia hali na kumkumbusha wajibu wake,na kwa sababu hii uhusiano wao umesambaratika kwa kuwa waliomwandikia wamekasirika,kwani hasira zilikuwa ndani ya barua zao zilizotaja waziwazi Afida ni msaliti wa ukoo wao. Kuna uhamaji wa Afida kutoka nyumbani kwa Bwana Bawa na Bi.Marneti na kwenda katika Taasisi ya lugha ya Peponi ili kusoma Kipeponi ambao ni usasa wa elimu.Lakini alificha sababu za muhimu zaidi za yeye kufanya hivyo kwa sababu Bi.Marneti alitaka kuondokewa na usumbufu wa kuuguza maradhi ya Afida asiyoyajua na kuondokewa na usumbufu wa kulinda mumewe Bw.Bawa hasihusiane na Afida.

### 4.9 Kubadilika kwa utamaduni

Uhamaji na maingiliano ya watu kutoka sehemu mbalimbali yanaathiri kwa kiasi kikubwa tamaduni za watu.Mathalan, wahamaji wa nchi yetu wanapoingia nchi nyingine wanapata tabia Fulani maalumu za kitamaduni.

Tabia hizi zilizoenea na kusambaa nchini uathiri tamaduni asilia za wahamaji kwani wanakumbana na mawimbi tofauti ya kitamaduni ambayo yanaweza kuwateka huku yakiathiri maadili yao.Katika mwagano wa Afida kuelekea Peponi, Shabani anamsogea Afida.Anatamani kumvamia na kumkumbatia lakini madhehebu ya utamaduni hayamruhusu.Angeweza kumkumbatia mbele ya mama mkwe,au mbele ya ndugu na jamaa zake Afida,ingawa wote walijua kwamba pana uchumba baina ya, (uk. 14).Lakini tunaona Afida anahamia Peponi na kuathirika na utamaduni wa Peponi na ndipo tunamuona akimrukia na kumkumbatia Neshboch na kumpa zawadi ya busu la kugandisha midomo yake kwenye midomo ya Neshboch,bila ya hofu yeyote kwa matakwa ya haja za kidumia, (uk. 148).

### 4.10 Hali ngumu za maisha

Afida katika usakaji wake wa elimu na hasa siku za mwanzo ni katika Taasisi ya Lugha ya Peponi.Hali inakuwa ngumu hasa kipindi cha baridi kinakuja na kero nyingi kwa kupindukia kiwango cha miaka hamsini iliyopita, (uk. 89).Wanafunzi wa Peponi wanamtenga na kumbagua wakidhani Afida si mtu ni dude tu,au labda mtu anayetoka mwezini.Inakuwa taabu kubwa kupata rafiki, (uk. 90). Anaishiwa na pesa za matumizi anazoletewa na Bi.Marneti.Hazitoshi kamwe.Kwani hazikuizima tamaa ya vitu inayozidi kujaa moyoni mwake, vingi anavitamani na anavihitaji na tama hiyo inamzidi nguvu ata ana kizuizi nayokwa ule mshawasha wake, (uk. 92).

### 4.11 Migogoro

Migogoro inazuka kutokana na Afida kutaka usasa na kusaka elimu na harakati zake za kuichumia familia yake Peponi.Na hivyo, kuna ugomvi kati ya Bi.Marneti na mumewe Bw.Bawa,ugomvi huu ulianza baada ya kuja kwa Afida nyumbani kwao na kusababisha kuharibika kwa uhusiano kati yao.Mgogano wa kwanza ulitokea mwezi mmoja tu baada ya Afida kufika Peponi na ulihusu wapi alazwe Afida. Bw.Bawa alisema lazima alazwe kwenye chumba chenye joto la kutosha kwasababu si uungwana kumlaza kwenye chumba kile chenye baridi ya kumtia mtu maradhi na tena lazima awekwe chumba cha karibu na wao,ili akipata shinda usiku wawe karibu pia kumnyooshea mkono wa msaada.Lakini Bi.Marneti alisisitiza

kwamba lazima alazwe huko mbali azoee baridi au,walau kwa muda mfupi,apelelezwe kama hana maradhi.Uk wa 30. Pia siku moja Afida akielekea chumbani kwake baada ya kukoga alisikia ugomvi wa Bi.Marneti na Bw.Bawa kuhusu wivu wa Bi.Marneti kwa Afida akidai alimtaka mumewe na hivyo alitaka apelekwe shule akasome, (uk. 41). Ugomvi huu unaathiri uhusiano wa Afida na shangaziye kwani Afida aliona maneno ya Bi.Marneti katika ugomvi huo kama matusi na simango na akalia sana.

**4.12 Unyama**

Bi.Marneti hajitumi wala kuhusiana na Afida katika kufanya kazi za nyumbani kama kuosha vyombo, kwa kuwa ana mashine za kutekeleza haya yote bila kuhitaji maingiliano ya binadamu. Ndani ya nyumba yake na Bw.Bawa mmejaa samani na vifaa vya haja na usaidizi kwa binadamu.Kwa mfano,kuna jiko kubwa lenye nafasi pana and ndefu, lenye kuzungushiwa makabati na rafu na meza zilizojengewa kutani,'*Cooker*', friji,buli ya kuchemshia maji,mashine ya kutayarishia tosti za mkate,mashine ya kuoshea vyombo,chombo cha kusagia vitu kama kahawa nafaka na vikombe vya aina nyingi, (uk. 27).Hivi vyote vinavyomondoshea binadamu udhia wa kujituma,bali hufanya kazi iwe rahisi na bora kwa kufanikisha mambo.Afida anakiri nyumbani humo mna ukamilifu wa mahitaji ya utamanduni wa kisasa wa vyombo na vitu visivyo na idadi au fikra utamaduni ambao siku zote hizi amekuwa akiutamani tokea alipokuwa kule kwao,ingawa bado mpaka sasa hajaukaribia maana yeye analazwa chumba cha baridi kama maiti.Ubinadamu wa Bi. Marneti umeathirika kwani anavitegemea vyombo hivi katika kutenda kazi kila siku anasahau kuwa Afida ni familia na hivyo binadamu mwenzake na si mashine wala chombo kwani katika, (uk. 30) anasisitiza kwamba Afida alazwe mbali azoezwe baridi katika chumba ambacho mitambo ya joto haifanyi kazi vizuri.Uhusiano wao na Afida unaanza kuathirika kwani hamjali, haoni kama baridi hii inaweza kumdhuru afya au kumtia maradhi na hata kumsababishia kifo. Unyama huu ulidhihirishwa na mwalimu wa somo la siasa alivyowaonya Afida na wanafunzi wenzake shuleni kuwa

> "vifaa vya wingi namna hio vinatufanya sisi binadamu tuwe wategemezi wa mashine katika kila kitu, hali ambayo inaelekea kuufuta ubinadamu wetu, (uk. 28).

### 4.13 Ubahili

Bi.Marneti kama mfadhili wa Afida akiwa Peponi ampi pesa za kutosha kukithi mahitaji yake tu (Uk. 85) anategemea pesa za kugaiwa na hizo si mpaka mtoaji atake bali atatoa kwa kulazimishwa, (uk. 105) alilipiwa vyakula vya bure na vinywaji na Yakrobich na Saparata kutokana na ubahili huu wa shangaziye hivyo kuathiri uhusiano wao.

### 4.14 Kutojali

Shangazi ya Afida Bi.Marneti tokea alipoondoka kwao Motoni miaka mingi iliyopita, ndio sasa anasikika anapomwalika Afida kwenda Peponi na amemwalika yeye tu, (uk. 5). Amesahau uhusiano wake na familia yake, hata hakuwajali walivyoishi kama ifanyavyo aila yao yote Motoni na katika utamaduni wa huko. Anazigatia utamaduni wa Peponi kwani wapeponi hawadhamini maingiliano ya familia,wao humtafuta mwanafamilia mwezake utakapo kitu kutoka kwake na uhusiano huu ndio umeigwa na  Bi.Marneti.

### 4.15 Mabadiliko ya lugha

Ni lugha yenye wingi wa mafumbo,istiara na kuchanganya ndimi kwingi.Mafumbo haya yana maana fiche.Istiara nayo imejitokeza kwa wingi kupitia mhusika mkuu na Bi.Marneti.Afida kama mhusika mkuu ni sitiari ya mwanamke aliyekaidi utamaduni asili na kushika utamaduni wa sasa.Mhusika Afida inambidi kulazimika kutumia maneno ya kiingereza ili kuonyesha hisia zake za maneno ya kisasa na elimu yake.

### 4.16 Umaskini

Familia ya kiafrika inaendelea kukandamizwa na wageni wanaotoka nchi za magharibi. Tunawona wageni wanaokuja Motoni wakinunua matunda yao kwa bei ya chini. Hawa ndicho wenye nguvu za kusema na wanachosema kitekelezwe ndio hutekelezwa.Utawala wao unaendelezwa kupitia vitendo vyao.

### 4.17  Maradhi

Kuna maradhi yale yanayotokana na tabia ya mtu binafsi mfano, ukimwi,saratani n.k.

#### 4.17.1 Ukimwi

Kati ya majanga yaliyokumba jamii ya kimataifa duniani.UKIMWI unatishia kuwa hatari zaidi.Kihistoria inahofiwa kuwa kufikia mwisho wa mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini na moja idadi ya wahasiriwa wa UKIMWI itazidi jumla ya wote waliongamia katika majanga yaliyotangulia.Njia kuu ni kupitia kwa kufanya mapenzi kiholela.Asilimia 75 ya maambukizo

hutokea kwa njia hii. Shuhuda anapatwa na maradhi haya kutokana na tabia zake za mapenzi ya kiholela na kama Afida anavyosema, Shuhuda amejitia katika majanga hayo kutokea alipofika Peponi kwani ameingia katika utamaduni mchafu, mpaka uchafu ukatishia uhai wake, (uk. 161). Ukimwi ni maradhi hatari kwani ndiyo yanayosababisha kifo chake.Katika hatua za mwisho kabla ya kifo cha hospitalini hali hii yake inaathiri uhusiano wake na Afida kwani Afida anapatwa na majozi mengi na kuathirika kisaikolojia.

Matarajio ya maisha ya wastani kupungua kutoka miaka sitini hadi thelathini na tano, kama anavyokufa Shuhuda akiwa bado kijana.

#### 4.17.2 Saratani

Kati ya magonjwa yanayowasumbua binadamu ni saratani au kansa.Kuna saratani za aina nyingi.Hata hivyo, saratani ya mlango wa kizazi ndiyo inayoongoza katika familia za Afrika. Lakini jambo la kusikitisha zaidi kuhusiana na vifo hivyo ni kwamba, vinaweza kuepukika kutokana na teknolojia ya kisasa ambayo inapatikana kwa bei nafuu. Kwa mfano, Afida anapogundulikana nayo akiwa Peponi anafanyiwa operesheni haraka na anapona, (uk. 185).Idadi ya wanaokufa kwa ugonjwa huo katika familia za kiafrika ni kubwa zaidi, kwani idadi hiyo ni mara tatu wanaokufa kwa ugonjwa huo katika nchi za Ulaya na Amerika ambako mipango ya uchunguzi wa mapema imepunguza idadi ya vifo vinavyosababishwa na kansa hiyo kiasi cha muongo mmoja uliopita.

Kansa ya mlango wa kizazi ni ya tatu kati ya aina nyingine za kansa duniani na pia inaongoza kwa idadi kubwa ya wagonjwa wanaokufa kwa kansa hiyo miongoni mwa wanawake katika nchi zinazoendelea. Taarifa ya hivi karibuni ya shirika la Afya Duniani (WHO) inaonyesha kwamba kadiri ya wagonjwa wapya 466,000 huugua kansa ya milango ya kizazi kila mwaka duniani. Asilimia 80 ya wanawake wanaougua ugonjwa huo wanatoka nchi zinazoendelea.Wasichana wenye umri chini ya miaka 20 ambao huanza kushiriki ngono wakiwa katika umri huo nao pia wako hatarini kupatwa na kansa ya mlango wa kizazi.Kwa mujibu wa maelezo ya shirika la WHO,viungo vya uzazi vya msichana chini ya miaka 20 kwa kawaida vinakuwa bado havijakomaa vyema na hivyo vinakuwa rahisi kuambukizwa aina mbalimbali za magonjwa yanayohusiana na viungo hivyo. .Afida anapatwa na ugonjwa huu, kutokana na uraibu wake wa pombe

> “Unamkaushia pesa ambazo sasa hanazo tena kwa vile Neshboch hakuwa na jukumu la kumlipa pesa za kukihudumia ki-Dinda.Kila pesa zilipokuwa zinamwishia aliingia katika mtego wa kukaribishwa ulevi na wanaume kwa mtindo wa nipe nikupe.Afida akawa hatoki tena kwenye baa kuwafuata wafadhili wake ambao nao walitaka kufadhiliwa. …Akabidi kuingia katika bwawa huria la kuogelea katika ngono,” (uk. 175-177).

Ngono hii ya kiholela ndiyo chanzo cha saratani kwa Afida, Hali hii inaathiri uhusiano wake na mwanaye kwani anamwacha mwanawe Mkombozi katika makao ya watoto na kumnyima malezi ya mzazi ili aweze kupata matibabu ya dharura hospitalini.

**4.18 Utandawazi**

Ni suala la kila mwanadamu siku hizi.Maendeleo haya ni mapinduzi yasiyo na kifani katika uwanja wa mawasiliano .Mahusiano ya wanajamii yameleta umoja na kufanya ulimwengu kuwa kijiji.Mahusiano haya yanajitokeza katika nyaja za siasa,sayansi,uchumi na utamaduni.Katika maendeleo haya lugha imekuwa chombo muhimu cha utandawazi na kila kundi la wanadamu hutaka lugha yao iwe mojawapo wa nyenzo za utandawazi. Lugha ya Motoni imeimarisha uhusiano baina ya taifa na mataifa ambao ni utandawazi kwani inafunzwa katika Chuo kikuu kwani ndio Saparata anoisomea na hata baadaye tunamwona akisafiri kwenda Motoni.Utandawazi huu umeathiri mahusiano.

Utandawazi wa uhusiano wa kimataifa una manufaa kwa upande wa elimu kwani msomaji au mtafiti anaweza kuzuru vyuo mbalimbali na taasisi mbalimbali za kiakademia ulimwenguni na kujiendeleza kielimu.Matatizo yanayopatikana kutokana na utandawazi nayo si haba.Suala la kifamilia linafaa kupigwa darubini.Familia nyingi zimepoteza utamanduni wao uliohifadhi heshima na utu wao.Badala yake, wanajamii hao wamefuata mielekeo potofu ya kigeni wanayoiona ni ya karne ya sasa na inayostahili kuigwa.

**4.19 Mawazo finyu**

Afida anapoingia shule anaathirika na fikra za usasa na kuanza kuzungumza namna mpya (isiyo yenye kama awali) upole kwani alipokuwa darasani,

> “Alisikiliza kila kitu kwa makini, alisema bila kujali makosa, bila kuona haya au aibu. Aliuliza alipokosa kujua. Alijibu ilipombidi ajibu,”(uk. 90).

Hapa athari anayopata ni yenye manufaa kwani  hali hii inamwezesha kuibuka bigwa katika Lugha ya Peponi na wa kwanza kutoka peponi tangu miaka kumi na tano iliyopita. Naye Daktari katika zahanati ya kibinafsi alipopelekwa Afida akiwa mgonjwa anaonyesha mtazamo wa wanajamii wa Peponi kuhusu familia za Afrika kuwa watu wengi katika familia nyingi za Afrika wanakufa kwa malaria,kifuakikuu au AIDS, (uk. 37) , anaona haya kama magonjwa makubwa sana na ndio maana anayalinganisha na kufa kutokana na mafua ya baridi Peponi.Hapa ni falsafa mpya ya wapeponi kuona familia za Afrika hazina uwezo wa kukabiliana na magojwa yoyote na ndiyo yanayowaagamiza.

Bi.Marneti ana fikra zinazotokana na nyakati za sasa zinazotokana na utamanduni wa kigeni (Peponi) kwani anaona kuwa Afida anaweza kuhusiana na mumewe ambaye ni mjomba wake Afida na anamwonya Afida kwa kutumia kisa cha macho ya Mwani. Anamwonya Afida asivutiwe na mumewe na fikra hizi za kisasa za bibi huyu ndizo zinazosababisha kuathirika kwa uhusiano wake na Afida kwani anapomwonya,Afida anapukutikwa na machozi mpaka pale anapokabiliana na daktari katika chumba cha usaili zahanatini katika ukurasa 37 kwani alihisi shangazi yake amemtukana na kumuumiza kwa kumwona nyang’anya manyung’unya.

Mzee dawamu, mwalimu wa Afida wa Fasihi alikuwa anaathirika na chamngamano za usasa ulikuwa na mtazamo chanya wa maisha ya wapeponi wakati wa majira baridi. Alipokuwa akisaidia wanafunzi wa darasa la Afida kulichaburua shairi la majira ya baridi peponi. Alidengua fikra zote za ubwanyenye sinazosisitiza uzuri wa theluji na usafi wa hali ya hewa ya majira ya baridi na vilevile kuonyesha uombolezaji wa washairi wa peponi kuhusu kukimbiwa na jua, ujoto, maua na ndege wazuri ingawa kwa kitambu Fulani. Na majira ya baridi na kujikuta ndani ya maisha yao wamejizungazunga na maguo, huku wanufunikwa na kiza na mgubiko wa mawingu kwa muda mrefu.  Theluji inayosahabisha tope na utelezi unaonwangusha wat wa mzizimo wa baridi unaopenya hadi ndani ya mifupa yao kama kisu kinachopekesha mwilini kwa maumiro makali, (uk. 61). Unaosambabisa ware na mjzo wa kisirani na huzuni mkero wa kila mtu anayekwenda wa kurudi au hata aliyelala kitandani.

Wapeponi wana mitazamo tofauti na ile ya Wamotoni. Wanasema wamotoni hawabadiliki ni wajinga, hawana elimu, ni washenzi kwa sababu ni maumbile yao, wameubwa hivyo, mtotoni

hawezi kuwa kuna wao. Mitazamo hii wanaiambiwa nyumbani, mtaani, kijijini, shuleni, vyooni, redioni, magazetini nakurenye televisheni bila kutaka kutambua sababu, ili wajisikie na kukubali yaliyopo kwao, mabaya na mazuri, (uk. 63-64).

Ukoo wa Afida unamwandikia brua kumuuliza hali na kumkumbusha wajibu wake. Afida anawajibu wachache tu,tena kwa nadra sana, (uk. 67). Jambo hili linaonyesha kuathirika kwa maangiliano kati yake na familia yao kwani wanakasirika, hasira wanazionyesha ndani ya barua zao zinazotaja waziwazi kuwa yeye ni msaliti wa ukoo, kwa kusahau ahadi alizowapa walipokuja kumuaga katika kiwanja cha ndege. Wanasisitiza ndani ya barua zao mara kadha kuwa Afida hajui kulipa fadhila. Afida anasema hakumbuki namna walivyomfunza alipoluwa kinyando. Jambo hili linonyesha kuwa Afida amebadili fikra na mtazamo wake kuhusu familia ni nini baada ya kufika peponi.Pia ukoo wa Afida hapa una fikra finyu na za kupotosha kuhusu maisha ya Peponi.Wanaona Peponi kama mahali penye nafasi nyingi za kazi zinazolipa ujira wa juu, mahali penye raha tele na ufanisi maishani.

### 4.20 Dawa za kulevya

Tatizo la dawa za kulevya ni moja kati ya matatizo makuu katika jamii zetu.Pombe ambayo inaweza kujumlishwa katika kundi panala dawa za kulevya imetumiwa kama burudani katika jamii kwa kipindi kirefu sana.Katika jamii za zama za leo, kuna shinikizo za kijamii na kitamaduni ambazo zinawafanya watu wengi kuishia kuitumia pombe au bia na kuvuta sigara.Utumiaji wake unaathiri anayehusika pamoja na jamii yake. Utumizi wa sigara umeweza kusababisha utegemezi wake kwa kiasi kwamba hawezi kutenda pasi kuitumia.Kwa mfano, tunaelezwa na Afida kuwa Miongoni mwa watu wanaoathirika kwa kiasi kikubwa na tatizo la dawa za kulevya ni vijan.Kwa nini vijana wanaathirika kiasi hiki?Utumiaji wa dawa za kulevya unawavuta vijana ambao wamo katika harakati za kuwa huru na kuusaka ujitambuaji.Baadhi yao wanaelekea kuamini kuwa dawa hizi zitawapa sifa muhimu za kujitambua kama ujasiri,kujiamini hisia za kuwa huru n.k. Ni katika hali hii ambapo elimu ifaayoni muhimu ili kusaidia kuwaelimisha wanaohusika pamoja na jamii nzima. Moja kati ya sababu kuu zinazochangia kuweko kwa tatizo la utumiaji mbaya wa dawa ni kuvunjika kwa muundo wa mshikamano wa kijamii ambao ni msingi muhimu sana.Ikiwa msingi huu uliotegemewa na wanajamii umevunjika, uwezekano kuwa baadhi ya wanajamii watashindwa kukabiliana na hali yao

mpya.Hawa watajaribu kusaka kimbilio Fulani kwenye dawa za kulevya.Hii kwao inakuwa kama njia ya kujipumbaza na kujihakikishia kuwa wanaweza kuikabili hali hii mpya.

Afida anapohama anakumbana na hali ambazo hakuzizoea katika tamaduni walimokulia. Matatizo yanayohusiana na ulimbukeni huo wa maisha ya mjini unaweza kumtosa mtu kwenye dawa za kulevya. Katika kiwango cha jamaa,matumizi ya dawa za kulevya,yanauathiri ushikamano wa umoja wao.Watumiaji wa dawa za kulevya wanazungwa na kurengwa na tabia yao kiasi kwamba haja za watu wengine ndio muhimu kwao.Anayehusika anaathirika kiafya na kisaikolojia.Jamaa yake nayo inateseka kumwona mwenzao akiangamia kutokana na kuzitegemea dawa za kulevyva.Mtumiaji aliyerengwa na dawa za kulevya huwa tayari kufanya lolote ili apate pesa za kununulia dawa hizo.Matumizi ya dawa za kulevya chuoni unachochea kuwapo kwa matendo yanayohusishwa nayo.Matendo hayo haya ni kama wizi,ukahaba,utovu wa nidhamu.

**4.21 Utandarithi**

Wale wanaohusudu utandarithi wanaamini kindakindaki kwamba utamaduni huu wa kilimwengu umeleta mlahaka mwema baina ya watu binafsi.Watu husikika wakidai ya kuwa aina hii ya utamaduni imepigisha mbele ustaarabu wa wanadamu ulimwenguni kote,haya ni katika maisha asilia katika familia za kiafrika.Lakini hatukumbaliani nayo kwani umeleta kukizana katika mahusiano ya familia kwani hata baada ya Afida kuuhusudu utandarithi kwa kuiga na kuufuata utamaduni wa Peponi,alikuwa amepata uraia na paspoti ya Peponi She-shaiza anamsimanga na kumtusi kumwita takataka jambo ambalo linaleta uzushi mkubwa kati yao na mwisho kuyasambaratisha mahusisno yao na mumewe Neshboch, (uk. 153).Kwa upande mwingine wakerekatwa wa tamaduni za kimsingi za mataifa na makabila mbalimbali ulimwenguni wanadai ya kwamba utandarithi umeleta maangamizi makubwa ya tamaduni hizo.Vilevile unaelekea kuangamiza lugha nyingi zunazofungamana na tamaduni hizo.Kwa ajili hiyo basi,utandarithi unasababisha kutovuka kwa utu miongoni mwa wanadamu wote ambao wamo mbioni kusaka pesa na kuneemesha ubinafsi.Pia utandarithi umesababisha kutovuka kwa adabu kwa vijana wengi ulimwenguni kote ghaya ya utovu.Huko kutovuka kwa adabu kuendelea,kemeta zahama chungu mbovu ikiwa ni pamoja na kuenea kwa UKIMWI kwa kasi ya kutisha. Shuhuda anazama katika tamaduni za Peponi kwa kuiga mavazi yao na hali yao ya maisha jambo ambalo linasababisha kufa kwake kwa ugonjwa wa UKIMWI.

### 4.22 Kuwa na fikira na mawazo mapya

Uvumbuzi mpya huweza kuzua mageuzi ya kitamaduni mabadiliko makubwa sana hasa mabadiliko ya kisayansi na teknolojia. Mabadiliko haya yanaathiri matendo mengi ya uhalisia wetu kwa sababu tunalazimika kuanza kuyaigiza mambo mageni.Mathalan,mitindo ya mavazi na mienendo ya watu,kuathiri na mawazo na fikira za wengine kutokana na matumizi ya tarakilishi,kuiga maadili,na matendo ambayo hayakuwako katika utamaduni.Katika hadithi ya mahusiano Afida aliyohadithiwa na babake alipokuwa hajavua makini.

“Babake alimwambia kuwa uhusiano wa buibui jike na dume ni uhusiano wa ajabu na hatari. Buibui jike ndiye anayejenga nyumba imara kabisa hata kuliko nyumba yoyote iliyowahi kujegwa duniani na binadamu. Lakini kwa upande wa mahusiano nyumba ya buibui ni dhaifu mno. Anapokwishaijenga nyumba yake buibui  jike, humkaribisha buibui dume alale naye. Mara tu buibui jike humchoma sindano ya sumu na kumuua mumewe,” (uk. 176).

Kutokana na Afida kuathirika na elimu ya Peponi inayamfungua akili yake na anagundua kwamba ndiye buibui jike aliyechomwa mwimba wa sumu na kufukuziliwa mbali na buibui dume ili ahagaike duniani kabla ya kukikabili kifo chake. Alimkubalia Neshboch miongoni mwa vijana wote kama Yakrobich, Neshboch ndiye vilevile alimpelekea kuvunja kiapo chake cha kutokuuza mwili wake ovyo.Afida anapokuwa Motoni anasema hana bahati lakini anapopata fursa ya kwenda Peponi kwa mwaliko wa shangazi yake Bi.Marneti anaiona hii ndiyo bahati yake,.kwa sasa anagundua kuwa mambo sivyo.

### 4.23 Maadili mema

Profesa Marjan ni msomi mwenye elimu hadi kiwango cha juu kwani ni profesa wa mwanzo kutoka Motoni kuja kusomesha Chuo kikuu cha Peponi.Licha ya usomi wake ni mwema na msafi wa roho.Haya yanajitokeza kupitia kwa maingiliano ya kuaminika na Afida.Alipoanza kazi Chuo kikuu cha Peponi na kumuona Afida(akianza masomo yake) alimchukua na kumpeleka nyumbani kwake na kumjulisha mkewe mama Maryam.Tokea siku hiyo alikuwa mzazi kamili kwa Afida,alimchukua Afida kama mtoto wake,anampa nasaha na fikra za kijituuzima, (uk. 158.Baadaye Afida anapopotea anamtafuta wakiwa na mke Maryam, hata miaka sita inaelekea kupita bado wanazidi kushidikiza polisi wamtafute, (uk. 191). Elimu hii ya

Profesa Marjan imeewaathiri kwa namna chanya anamjali Afida kama familia hasa kwa sababu ametokea sehemu karibu na Motoni,bado anaiga namna ya mahusiano kama yalivyo katika sehemu aliotoka.

Mama Maryam licha ya kuishi Peponi kwenye utamaduni wa kigeni hajaathirika na usasa huu.Hii ni kwa sababu Afida anatueleza kuwa Mama Maryam ni familia kwa Afida kuliko Bi. Marneti kwani Afida anapomwarifu amepata ujauzito wa pembeni na hivyo ingembidi aache Chuo kikuu kwa muda,mama Maryam anajawa na uchungu wa mwana na mama mzazi,na machozi yanamtoka na hata anataka kumsaidia kumlea mwanawe Afida hadi awe mkubwa, (uk. 158). Maingiliano yao ni ya karibu sana kuliko yake na Bi.Marneti kwani Afida anasema,

> "Mama Maryann nilimwamini kwa kila hali kuliko shangazi yangu Bi.Marneti".

kuna elimu ya falsafa hasa falsafa ya maisha anayoipata kwa babake.Elimu hii inampa ujuzi kamili.Anapata kuelewa kuwa mwelekeo wa mtu wa maisha unatokana na nafsi yake ya ndani kabisa inavyohisi na uamuzi utakaoyoyafanya.

### 4.24 Kuboreka kwa mawasiliano

Kulingana na falsafa ya mawasiliano,kuna mawasiliano baridi na mawasiliano joto.Mawasiliano baridi ni kati ya watu wawili au zaidi na hayahusishi sauti au kukabiliana ana kwa ana.Mifano ya aina hii ya mawasiliano ni nyaraka zinazotumiwa kupitia kwa shirika la posta na magazeti yanayochapisha habari kutoka pembe zote za dunia.Kupitia mitambo ya tarakilishi na rununu.Njia ya pili ya mawasiliano ni mawasiliano joto.Katika aina hii ya mawasiliano wahusika wanazungumza wakikaribiana kwa sauti wakitumia lugha ya kuelewana.Vyombo vya mawasiliano vinavyoendeleza haya ni rununu,runinga,redio,mtandao na vinginevyo.Kwa mfano,kuna utumiaji wa rununu kama itumiwayo na Afida kuwasiliana na Shabani na inamwathiri vibaya kwa sababu bila matayarisho yoyote moja kwa moja anaelezwa kuwa yeye Shabani yuko chumba cha watu mahututi akiwa katika hali mbaya.Njia hizi za mawasiliano zimefaidi sana na kuleta maendeleo katika ulimwengu kwa jumla zimeleta uhusiano bora kati ya watu wa familia,nchi na mataifa mbalimbali.kisiasa,kijamii na kiuchumi.

Kutumia ndege kama aina mpya ya usafiri,ni njia ya mawasiliano inayofanya maisha ya binadamu kuwa mepesi na yenye furaha.Kutumia aina hii ya usafiri kunaipa koo ya Afida wakati

murwa wa maagano kwani wote kwa pamoja wanapata fursa ya kila mmoja kutoa maagizo kwa Afida na kunywa soda na kipande cha keki huku akiwapa ahadi kwa upande wake kutimiza matakwa yao na ya familia.Kujumuika pamoja hapa kunawaunganisha wanajamii na pia kusaidia kuimarisha uhusiano miongoni mwa wanajamii, (uk. 6).Peponi Afida ana magari ya kutembelea modeli mbalimbali yaliyokuwa huru kwake kuendeshea ukurasa wa 165 naye Bi.Marneti anatumia gari aina ya *Audi* kumpeleka Afida zahanatini, (uk. 35). Maendeleo upande wa mawasiliano yanahakikisha kuwa watu wanaoishi mbali wanawasiliana haraka sana na kuondoa tatizo la ukiwa.wanaweza kufanya hivi kwa kutegemea simu.

**4.25 Hitimisho**

Katika sura hii tumechunguza na kubainisha athari za usasa kwa familia za kiafrika na changamoto zinazoibuliwa na athari hizi na kupata uelewa kuwa,mwingiliano wa kifamilia ni muhimu sana. Kwa sababu baada ya Afida kupoteza ki-Dinda ndipo anapopoteza moyo wake na anapogundua hivyo akielekea katika baa ya “the lost” anapata jawabu au uono mpya, na anaamua kupata mtoto mwingine.Na anapokutana na Saparato kwenye “the lost” anamkubalia uhusiano wa mapenzi siku hiyo na anapata mtoto anayeitwa Mkombozi. Uhusiano huu wa kifamilia una msukumo wenye nguvu sana kwani kuzaliwa kwa Mkombozi kulimfanya Afida akate ulevi moja kwa moja kwani sheria ya Peponi haingemwacha mama mlevi alee mtoto ndani ya taathira ya ulevi wa kupindukia.Moja kwa moja uingiliano huu na mwanawe Mkombozi unamletea athari chanya kwa maisha yake kwani anabaadilika kuwa mzazi mwenye kumjali mwanawe na kumkidhi mahitaji yake kwa kila hali.Usasa tuliozungumzia kwenye sura hii ndio umechangia Afida kufikia hatima yake ya kushindwa na maisha yake na kutokomea na kumwacha mwanawe.

# SURA YA TANO

# MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii tunaeleza matokeo ya utafiti wetu kulingana na matarajio tuliyokuwa nayo na ni yapi tungetaka kupendekeza ili yatafitiwe zaidi na kwa kina ili pawe na ufahamu zaidi wa tuliyoyatafitia. Vilevile tutathibitisha iwapo madhumuni ya utafiti yalifaa katika kutuongoza ili tuwe kwenye mkondo wa utafiti wetu.

### 5.1.1 Kutathmini madhumuni ya utafiti

Madhumuni ya utafiti yaliyotupa mwelekeo katika utafiti wetu yalikuwa matatu. Kwanza ilikuwa tubainishe jinsi mwandishi wa *Mhanga Nafsi Yangu* alivyoshughulikia uhalisia na usasa wa familia za kiafrika.Hili limefaulu maana tumepata matukio mengi yanayorejelea uhalisia na usasa tulionao na wa hivi punde.Aidha mhusika mkuu amedhihirisha sifa nyingi kwa mkabala wa uhalisia na usasa.

Mawazo yake na maamuzi yake katika uhusiano wake na familia yao ni baadhi ya mambo yanayouiana na usasa. Nayo ya pili imetuongoza kudhihirisha maswala yanayopewa kipaumbele katika riwaya teule.Katika sehemu hii tumeweza kuthibitisha maswala haya ni mitangusano au mahusiano katika familia.Hivyo tumeonyesha uhalisia na usasa katika familia za afrika. Madhumuni ya mwisho ya utafiti yalikuwa kuchunguza na pia kuweka wazi baadhi ya changamoto zinazoibuliwa na athari za usasa kwa familia za kiafrika. Changamoto hizo tumezisawiri kwa kutoa mifano zaidi na kumwonyesha mhusika mkuu Afida alivyopambana na changamano za usasa ili kudhihirisha kuwa, kuna uwezekano wa mitagusano ya familia kufaulu iwapo haitaathirika na usasa kwa njia hasi.Hata ikiathirika, kuna uwezekano wa kujinasua kwa kurejelea uhalisia wa kiafrika.

### 5.1.2 Ujumla wa utafiti wetu

Utafiti wetu umekuwa wa maktabani na umehusisha kusoma kazi nyingi zinazohusiana na mada yetu ndipo tukawa na ufahamu wa yaliyotafitiwa na wataalamu wengine. Aidha tumeweza kupata data kuhusiana na swala la utafiti wetu kwa kurejelea *Mhanga Nafsi Yangu* ya S.A Mohammed .

Swala letu la utafiti lilikuwa limelenga kubainisha jinsi mwandishi alivyoshughulikia uhalisia na usasa wa familia za kiafrika kwa kuonyesha tofauti iliyopo kati ya uhalisia na usasa wa familia za kiafrika na kutambua kuwa kuna umuhimu wa kwenda na wakati kwa familia zenye kutawaliwa na utamaduni.

Katika hali hii tumeweza kuona  namna msanii alivyofanikiwa kusawiri familia za kiafrika kwa sifa zinazouiana na usasa na pia kuthibitisha kuwa riwaya inasawiri na inarejelea masuala ya mitagusano katika familia ya kiafrika na ina sifa za kuathirika na usasa wenyewe ambao ni pamoja na vile matukio yalivyoundwa, mandhari na pia wahusika. Utendakazi wake kulingana na usasa tumeushughulikia ipasavyo na huku tukifafanua kwa kina changamoto zinazoibuliwa na athari za usasa kwa familia ya kiafrika.Changamoto hizo zimechangiwa kwa pakubwa na masuala ibuka ambayo yamesababishwa na kuibuka kwa aina mpya za mahusiano. Mwishowe tumedhihirisha kuwa kufaulu kwa mhusika mkuu baada ya kuathirika na usasa katika mitagusano yake kumechangiwa na mikakati ya kisasa hasa falsafa za maisha mpya anazojiundia baada ya kuathirika na usasa wa usomi,tamaduni za kigeni,pamoja na kuongozwa na dhana ya maadili ya kiasili. Vilevile athari anuwai zinazoendelezwa na usasa katika mahusiano anaweza kupambana nazo na anaibua mbinu za kujisaidia kutokana na kufinyiliwa na dhuluma hizo. Ni wazi kuwa dhuluma hizo zinaathiri familia za kiafrika.Hapo ndipo tunapoona msingi wa nadharia yetu ya uhalisia ikilenga shabaha juu ya suala hili kwani athari zinazojitokeza katika utafiti wetu zinamulika familia za kiafrika. Mathalani jamii kutweza usasa bila kujali matokeo na jinsi yatakavyomwathiri mwanafamilia au hata kukosa uono wa kuwa unaathiri mahusiano katika familia hasa mshikamano wa ukoo, kwa namna chanya au hasi.

Hivyo nadharia tuliyoitumia imetupa mwongozo tosha wa tuliyonuia kutafiti. Mhusika mkuu anapotambua kuna kuenda na wakati ambao ni usasa, aliamua kuzinduka na kuukubatia lakini anapambana na athari za changamano za usasa zinazofinyilia mahusiano katika familia. Katika kupambana kwake amedhihirisha mambo ya kimsingi katika kuhusiana ambayo kila mwanafamilia anapaswa kuwa nayo iwapo ananuia kufaulu. Mambo hayo ya kimsingi ndiyo yaliyompa nguvu mpya na zaidi katika kutimiza.

## 5.2 Mapendekezo

Tunapendekeza utafiti zaidi ufanywe ili kuona iwapo kuna vipengele vya utamaduni vinavyoathiri mahusiano katika familia na kama vipo na ni kwa nini vinaendelezwa kwa wakati wa sasa.

Kando na tunayoyashuhudia tunatumai kuna mengine mengi ambayo yanaweza kutekelezwa katika familia za kiafrika zaidi kulingana na maendeleo yanayoshuhudiwa kwa sasa.Tunatumai utafiti utafanyika hata nje ya maktaba na nje ya fasihi ambapo hali halisi itajitokeza wakati familia zitahojiwa kulingana na ufanisi wake na zinavyopambana na usasa maana teknolojia inayoshuhudiwa hivi sasa haijaacha familia nyuma. Suala muhimu analopasa kukumbuka binadamu ni kuwa ana wajibu wa kuitawala teknolojia lakinisiyo kiacha teknolojia yenyewe imtawale.Lazima mahusiano yake na binadamu wengine yatawaliwe na utu na ubinadamu wala si ubinafsi na kujiona bora zaidi ya binadamu.

**MAREJELEO**


Beard na Verma, (1981) katika Judith, B.(Mhariri) "*Doing your Research Project*"*A Guide For First Time Researcher in Educationand social sciences*. Milton Keynes, Philadephia Open University Press, Philadephia.

Boyle, N.& M. Swales. (1986) *Realism in European Literature*. London: Cambridge University Press

Caleb, C.W. (2013). *Taswira ya mwanamke* katika Tamthilia za *Nguzo Mama na Mama Ee*.Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njogu,K. (1986*)*. "Falsafa ya Shaaban Robert katika Riwaya zake" Katika *Mwamko* Jarida la Chakina (limehaririwa na mwandishi mwenyewe) Chuo Kikuu cha Nairobi

Fokkema, D. (1997). *Theories of Literature in the Twentieth Century*. London: C. Hurst and Company.

Forster, E. (1927). *Aspects of the Novel*. London: Penguin Books.

Lukacs,G.S. (1963). *The meaning of Contemporary Realism*. London; Merlin Press.

Hegel,G.W.F (1979). I*ntroduction to Aesthetics;* Oxford: Clarendon Press.

Karoki E. (2014*)*. Suala la uhamaji na uhamiajikama linavyoendelezwa katika riwaya ya Mbali na Nyumbani ya Adam Shafi. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.

Margaret,M. (2014). Uhakiki wa maudhui na mtindo katika Tikitimaji. Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.

McNeil,W.H. & Adams,R.S. (1978). *Human Migration:Pattern &Policies*. Bloomington: Indiana University Press.

Mbatiah, M. (2001): *Kamusi ya Fasihi***.** Nairobi: Standard Textbook & Graphics and Publishing.

Mohammed, S.A. (1990) *Tata za Asumini*. Nairobi: Longhorn.

________________ (2010) *Nyuso za Mwanamke*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Ngara E. (1985). *Art and Ideology in the African Novel*. Nairobi: Heinman.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki Wa Kazi Za Fasihi*. Augustana College: Rock Island, IL 61201.

Robert, S. (1967). *Kufikirika*.Nairobi niversity Press.

Robert, S. (1991). *Maisha Yangu Na Baada Ya Miaka Hamsini*. Mkuki Na Nyota Publishers: Dar Es Salaam.

Senkoro,F.E.M.K. (1982). *Fasihi*.Dar.es.salaam: Press ana Publicity Centre.

Shafi,A.S, (1999). *Vuta N'kuvute*. Mkuki Dar es Salaam. Na Nyota Publishers.

Shihabuddin C. na Mathias E.M (1977) *Historia ys Kiswahili*.Oxford University Press. Dar Es salaam.

TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* . Daressalaam;

_______________ (1999) *Nguvu ya Sala*, Nairobi Longhorn Publishers.

________________ (2006). *English-Kiswahili Dictionary*: 3rd Edition. Dar es Salaam.

Wamitila, K. (2003).*Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi : Phoenix Publishers.

_________________ (2005). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

_________________ (2006). *Uhakiki wa Fasihi Nadharia na Misingi yake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

_________________ (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi***.** Nairobi: Vide-Muwa & Publishers Ltd.